

MASWALI NA MAJIBU



Ndipo kama...lakini ni katika kanisa hili tu. Nami nikawaza, “Nikifundisha katika usiku wa kwanza, kanisa lilivyo siku hizi...na wakati, kigeografia, katika Biblia, mahali ambapo tunakaa, basi kanisa bila shaka litakuwa macho. Ndiposa ninene juu ya *Ile Chapa ya Mnyama*, nao waone hio ni nini. Ndiposa *Ule muhuri wa Mungu*, hayo halisi na kinyume sasa, hayo ni giza na Nuru sasa, hayo ni ndani au nje sasa, na hilo ndilo jambo muhimu sana kufundishwa sasa.”

² Nami nawaambieni, marafiki, nasema hili kwa moyo wangu mbele za Mungu, kinyenyekevu, sijawahi kusikia...ule upako wa Roho Mtakatifu kunena maneno niliyonena katika usiku mchache uliopita. Naam. Lakini umenikulia mwingi. Nami ningeenda nyumbani, hata singelala baada ya kufika nyumbani, upako mwingi sana.

³ Sasa, nimeyatupatupa haya nje hapa huku nikitumaini ningeipata jambo mahali fulani. Ona? Kupata ma—mawazo yote ya watu katika kipande cha karatasi hapa. Kama nisipopata hili hivyo, na Bwana asiponifunulia, nitaendelea hadi nilipate. Na Mungu atanipa. Naam. Na kwa hivyo tunapolipata, huenda ikawa ni shoka ndogo, zee lililozikwa mahali fulani, lakini Akani alikuwa na moja, pia. Mwajua, yatupasa kuondolea mbali kitu hicho, ndipo tutaendelea na kusonga mbele katika Ufalme wa Mungu.

⁴ Basi, Bwana awabariki. Na sasa kabla hatujafungua Neno... Na sasa-sasa, kila mmoja wenu ana shule ya Jumapili asubuhi. Bila shaka, una...Si-Singewaambieni msihudhurie shule zenu za Jumapili, huo ni wajibu wako kwa kanisa lako. Naam. Lakini, sasa, usipoenda kwa shule ya Jumapili, njoo na utuone sisi asubuhi. Ndiposa iwapo kanisa lako halina ibada kesho usiku, Jumapili, umealikwa, tutafurahi kuwa nawe wakati wo wote. Na kwa hivyo Bwana awabariki. Na salimieni Wakristo wote kwa niaba yangu, siji hapa sana.

⁵ Nilikuwa tu nikitazama chumbani mle, kijikaratasi nilichokiandika mle bado kimewekwa hapa kama ukumbusho kwa kanisa hili. Nami nilisema, “Bwana ananiita nje,” nanyi nyote mlilia na kuomboleza. Nakumbuka usiku wa kwanza nilipoondoka. Mwakumbuka wito wangu wa kwanza, ye yote humu? Ninyi mlichanga pesa kunituma St. Louis, ambako maskini Betty Daugherty aliponywa. Nalika... .

⁶ Kumbuka, niliomba kabuti la mtu fulani hapa nivae. Sikuwa na koti lo lote la kuvaa. Nami nalienda kule na kuketi katika kiti kikuukuu cha motokaa kuenda kule St. Louis. Mwakumbuka Wakati huo? Nami niliomba moja ya makoti ya ndugu, lilikuwa

kubwa sana kwangu, nilibeba mkononi mwangu; kwa sababu ilikuwa baridi nami sikuwa na koti.

⁷ Ndiposa tukaenda kule, nami nilienda St. Louis na nikakutana na Ndugu Daugherty kule. Binti yake mdogo, madaktari wote kule, na wataalam na mahospitali walimkatia tamaa. Yeye alikuwa kama wazimu kaidi sana. Wahudumu kote mjini walikuwa...kila mahali, ndani mle walikuwa wakimwomba. Nami niliingia na kumwomba na maskini watu hao walionekana wenye huzuni sana. Na msichana yule mdogo ndani mle, akipiga mayowe na kulia, akipigana.

⁸ Na—naye hangetoa sauti kama mwanadamu tena, ilikuwa kama ya mnyama, alipwewa sauti sana kwa...lo, yapata miezi mitatu minne. Ilikuwa ni ugonjwa wa ngozi ya uti wa mgongo au...la, dege, katika—katika uti wa mgongo. Na midomo yake midogo yote ilikuwa imeliwa, ikitokwa damu. Na vidole vyake vidogo vikitokwa na damu kote alikoendelea kuuma vidole vyake, na mambo kama hayo, na kulia kwa sauti kuu na kuendelea.

⁹ Nami niliomba, nikaenda kanisani. Nikangoja masaa baada ya masaa. Nikiketi katika hilo gari zee na kungoja. Singeacha ugojwa huo hadi nisikie toka Mbinguni. Nikiketi tu pale ndani ya motokaa, ono lilinijia, kasema, “Enda kamwambie huyo baba na baba yake.” Kasema, “Tazama...Mwambie mwanamke huyo kwamba hivi majuzi, kule mjini, alinunua birika ndogo nyeupe. Haijawahi kutiwa maji hapo kabla.” Na kasema, “Mwambie atazame katika saraka ya tatu naye atapata leso kwenye karatasi, ambayo haijatumiwa bado. Mwambie ajaze maji. Msimamishe baba upande wako wa kuume, na babu upande wa kushoto, na mkakariri, ‘Baba yetu aliye Mibinguni...’ Na muanzapo, mwache kidogo...mpanguse uso kwa hiyo leso. Ndipo katikati ya maombi hebu huyo mwanamke anguse mikono, kisha miguu. Ndipo simama na kusema, “BWANA ASEMA HIVI”

¹⁰ Mwajua kilichotendeka, sivyo? Yeye aliponywa papo hapo. Nasi tulishikana mikono na kutembea barabarani na tukanywa soda pamoja. Naam. Hiyo ni kweli. Ilichoea St. Louis. Katika mikutano yangu kule, elfu kumi na nne usiku wa kwanza. Hiyo ni kweli. Katika Saint...

¹¹ Ni vibaya sana kuwa niliacha hayo; kuenda tu kuwafanya waanze kuja mstarini, mmoja baada ya mwingine, baada ya mwingine, baada ya mwingine. Kuingia tu katika nyumba na kuketi hadi imekwisha, na kurudi nyumbani, naamini hilo lingekuwa heri katika yote...mikutanoni.

¹² Vema, hebu na tuinamishe vichwa vyetu hali tukinena na Mwandishi wa Neno hili, sasa:

¹³ Kwa hisani ya Bwana wetu Yesu Kristo, tunakujia Wewe, Baba yetu. Na katika Jina Lake twaomba rehema za

Kiungu kuwa Wewe utatusamehe dhambi zetu na makosa yetu tuli yokukosea Wewe. Na kama kuna dhambi yo yote katika kanisa hili ndogo usiku huu, twaomba, Bwana, kama—kama mtumishi ninayesimama hapa, kama mchungaji juu ya kondoo (kama Biblia ilivyosema, “Chunga kundi ambalo Roho Mtakatifu amekufanya mwangalizi, upate kulilisha”), na sasa, Baba, nawaombea hao, kuwa Wewe utawabariki na kuondosha dhambi zao zote. Ponya magonjwa yao yaliyo kati ya watu. Na, Baba uliye Mbinguni, naomba kuwa rehema Zako zitakuwa juu yetu sasa.

¹⁴ Hapa, mbele yangu, kumewekwa makaratasi yaliyoandikwa, toka katika nyumba nyingi na watu wengi, mna mahitaji, maswali ya kindani sana ya Biblia yanayozidi elimu ya kawaida. Nasi twahitaji msaada Wako, Bwana Yesu. Na nimeyachukua haya sasa hivi, nikaingia chumbani mle, nikaomba, nikatoka, nikayatenganisha hapa, na kuyaweka yapaswayo kujibiwa sasa upande mmoja, na mengine yanayohitajika kuendewa Maandikoni, upande mwingine. Hivyo ni kadiri ni juavyo wakati huu, Bwana.

¹⁵ Nami naomba kuwa tokea hivi sasa utatuongoza toka hapa na kuendelea, na upake mafuta watu Wako humu usiku huu, mdomo wa mnenaji, na masikio ya wasikizaji. Na Roho Mtakatifu aje na ashike Neno sasa na aliingize moja kwa moja katika kila moyo, na lipokewe katika roho wa upole, na litolewe vivyo hivyo. Na, ibada ikwishapo usiku huu, na turudi nyumbani, tukisema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu kwa sababu ya Uwepo Wake na baraka Zake?” Bwana, bila kujua la kusema, najikabidhi mwenyewe Kwako na maswali haya, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya majibu. Amina.

¹⁶ Asanteni, marafiki, kwa utulivu wenu. Najisikia heri. Yaonyesha tu yale wengi . . . wengi wa maswali haya ulivyokuwa.

Ndungu Bill, tafadhali endelea juma linalokuja lote.

Tafadhali kaa juma lingine.

Tadhali kaa zaidi kidogo.

Ndugu Bill, tafadhali kaa juma linalokuja, zaidi kidogo, nafsi zetu zina njaa kwa ajili ya Chakula aina hii.

Je, kanisa hili hufundisha kuwa . . . Hilo lilianguka tu ndani mle, hapo si mahali pake.

Nina wavulana wawili, umri wa miaka miwili . . . Hilo . . . Nimeyachanganyisha, nadhani, juu ya hili. Ona? Hapa, heri nilipeleka juu hapa, pia, hilo linahusu mambo ya kibinafsi.

Ndugu Bill, waweza—ungependa juma moja zaidi? Tungependa juma moja zaidi la mafundisho haya ya Injili.

Ombi langu ni kuwa ukae juma lingine. Ningependa sana ukae zaidi kidogo, wajua sisi kila mara . . . twaweza kujifunza mengi zaidi kila mara.

Sasa, waweza kukaa juma moja zaidi, tafadhali?

Ndugu Bill, tafadhali tuhubirie juma moja zaidi hakika tunayahitaji sana.

Ndugu Bill, ombi langu ni kuwa Mungu atageuza nia yako na akufanye ukae juma lingine.

Swali langu ni: **Vile visahani virukavyo angani ni nini, je hivyo ni vitu vinavyotoka kwa Mungu kama ishara? Nami nakusihi ukae juma moja zaidi.**

Tadhali kaa juma lingine moja.

17 [Ndugu Branham aongea na Ndugu Neville—Mh.]

18 Sasa, hapa kulikuwa na mwingine aliyesema...ninge... ni—ninathamini maombi haya. Na Mwenyezi Mungu aliye Hakimu wangu, nikisiamama hapa sasa katika mahali hapa patakatifu...kabla sijaondoka nyumbani, Roho wa Bwana aliniambia, akasema swali hili litakuwa humu. Nami sikujua cho chote kulihusu, lakini nilijua lingekuwako hapa:

Je, Mashahidi wa Yehova ni dhehebu la uongo?

19 Ona, mtu fulani...Na Roho Mtakatifu, mahali pale... nikisimama katika chumba changu cha kuogea, kabla sijakuja humu; Mungu ambaye ni Hakimu wangu hakika aliniambia, “Hilo litakuwepo jukwaani,” na kusema, singesema “lo lote kulihusu, niendelea tu.” Ona? Ona? Kwa hivyo, mimi...Mwajua yale niliyosema usiku uliopita, sivyo? Vema, hivyo ndivyo ilivyokuwa.

20 Vema, sasa tutaanzia juu hapa kwa baadhi ya haya.

21 Sipiendi kutaja kitu cho chote, na kutaja mtu fulani au mtu binafsi hivyo. Napenda tu kulifundisha katika njia fulani tu... kulitupa jambo lote pamoja. Na—nanyi mwafahamu, sivyo? Kama ningesimama hapa na kusema, “Sasa, Ndugu Neville ni *hivi na hivi* na jambo *fulani*”...Kama ningalimnena vile, ningeenda nyumbani kwake na nimwite nje na niongee naye kuhusu hilo. Ona, ni—ningemwambia Ndugu Neville.

22 Lakini, sasa, hapa kuna maswali kadha, sijui nianzie wapi, ni kundi layo tu yamewekwa hapa. Linasema:

25. Ni uhusiano gani uliomaanisha ambao kanisa Protestanti linao na kanisa Katoliki?

26. Nini maana ya “ile sanamu mnyama?”

23 Sasa, hilo lilikuwa baadhi ya maswali toka...uliopita... labda lilikuwa kwa...Sasa, nitajaribu niwezavyo, kwa msaada wa Mungu, kuyajibu vema kadiri nijuavyo. Sasa kama Yeye atanipa maarifa, kwa sababu Mungu ajua kuwa nili—niliyachukua tu, hapa jukwaani.

Sasa, uhusiano gani uliomaanisha ambao kanisa Protestanti linao na kanisa Katoliki?

²⁴ Sasa, nitajibu hilo kwanza, Mungu akinisaidia. Nilisema kuwa kanisa Katoliki lilikuwa... Twaona kuwa ile chapa ya mnyama, usiku wa juzi, ilipasa ije kutoka Rumi. Sivyo? Haiwezi kutoka nchi nyingine ila Rumi. Hapo ndipo imekaa, hapo ndipo imewekwa. Nami nilisema sina lo lote dhidi ya Wakatoliki, sina lo lote dhidi ya ye yote, sisi sote tu viumbe tunaokufa tunaajaribu kwenda Mbinguni.

²⁵ Papa ndiye mtu afundishaye, yule askofu mkuu wa Canterbury ni mwingine, na mwingine, na mwingine, na mwingine; nami ni mmoja wa waalimu, hivyo tu. Wao wangefundisha na kusema, labda, nilikuwa shupavu wa dini na nilikosea na kadhalika. Nami nina haki... kama naweza kulithibitisha kwa Maandiko. Au kama wao wanaweza kuthibitisha kwa Maandiko kuwa mimi ni shupavu dini, basi mimi ni mshupavu, lakini kama naweza kuthibitisha kwa Maandiko kuwa wao wamekosea katika mipango yao, basi ni kosa, Maandiko yako sahihi. Nanyi hamna mahali hata pamoja sasa, yapasa yaje kote katika Biblia, kila mahali.

²⁶ Sasa, nilisema, “Kanisa Katoliki lilikuwa kanisa mama,” na hilo ni kweli hasa. Kanisa Katoliki ni kanisa mama, inapofikia mipango ya kanisa. Kanisa Katoliki lilikuwa kanisa la kwanza lililoundwa; yapata karibu... historia bora sana mliyo nayo, yapata A.D. 606, mahali fulani ndani mle wakati wale makasisi wa mwanzoni, zamu ya pili au ya tatu, ya mitume. Wao walikuwa wamekufa na wakaanza kutengana katika vikundi vidogo-vidogo. Na Warumi, walipoongoka, Milki ya Kirumi ikatawala taifa, na ndipo kanisa na taifa viliungana pamoja na kuanzisha dini iliyoitwa “Dini ya Dunia Nzima.” Neno *Katoliki* maana yake “dunia nzima.” Walitengeneza kanisa, ambao ndio wakati wa kwanza ambapo dini (dini ya Kikristo) iliwahi kuwa dhehebu katika historia yote ya ulimwengu.

²⁷ Dini ya Kiyahudi haikuwahi kuwa dhehebu kamwe, ilikuwa watu huru. Walikuwa na makanisa bali, hawakuwa na dhehebu. Mungu wao alishughulikia taifa, si dhehebu. Ilikuwa ni taifa.

²⁸ Na sasa, ndiposa kanisa Katoliki lilikuwa ndilo dhehebu la kwanza. Ndipo tuliyachukua hayo katika Biblia kuona dhehebu hilo lilikuwa gani. Na kulingana na Neno la Mungu, lilipaswa kusimamiwa na mtu mmoja, mtu mmoja. Na mtu huyo alipaswa awe katika kanisa linalokalia milima saba katika Rumi, kulingana na Biblia. Hakuna... Naye alipaswa kuwa na nguvu za kutawala katika kila taifa ulimwenguni, mamlaka ya kidini. Hakuna lingine ulimwenguni.

²⁹ Na—na Ukomunisti, tuliona, sio—sio upinga-Kristo ambao Yesu alinena. Ukomunisti si—si taifa kama Urusi, Ukomunisti ni pepo. Amerika imeliwa naye. Ako katika makanisa, ako ndani ya watu, ako katika biashara, ako kila mahali (Ukomunisti ni pepo yake), ako katika shule, ako manyumbani, kila mahali.

³⁰ Na ndipo—ndipo walipofanya kanisa hili dhehebu ambalo lilikuwa kinyume. . . Na sasa tumehubiri zile Nyakati Saba za Kanisa, na unabii, jinsi hasa Mungu alizileta kote katika Biblia hapa kwetu sisi. Nasi tuliona kwa historia na Biblia, kuwa kila wakati uliwadia tu kulingana na Biblia, kulingana na historia; kila mmoja uliingia kwa wakati ule ule, kote katika nyakati za giza. Na ndipo kanisa Katoliki liliundwa katika ule Wakati wa Giza.

³¹ Kisha matengenezo yakaingia, ambayo ni Martin Luther. Na Martin Luther alikuwa na nuru, ile nuru kuwa, “Wenye haki wataishi kwa imani, kuhesabiwa haki kwa imani,” katika yale—katika yale matengenezo. Kasisi Mjerumani aliyekana na kusema kuwa kule kupokea ushirika yeye alipoushika. . . Nao walipaswa kusema, “huu *ni* mwili wa Kristo,” naye akautupa sakafuni na kusema, “Huu *si* mwili wa Kristo, huu ni mkate mwembamba!” Na kwa hivyo yeye akakataa kanisa Katoliki katika kufanya hivyo, na kutoka kwake katika yale matengenezo ya mwanzoni. Martin Luther alifanya hayo, na hilo lilikuwa tendo la ajabu.

³² Basi, hata hivyo, mahali Luther alikosea, Luther aliunda kundi lingine la dhehebu kama tu vile kanisa Katoliki lilivyofanya, aliwaunganisha watu.

³³ Ndipo, moja kwa moja, kukaja nuru mpya. Na wakati nuru mpya ilipokuja, Mungu akaondoka na watu Wake. Watu waliojiundia dhehebu katika kanisa la Kilutheri, iliwapasa wakae na kanisa lao ili wawe na. . . Hivyo ni kama tu Wakatoliki walivyopaswa kuwa, lakini Wakatoliki wengi waliondoka na wakawa Walutheri. Vema, kisha Wesley alipokuja na ujumbe wa utakaso, ndipo Walutheri wengi hawangeacha kanisa lao; lakini wengi wao walifanya hivyo, na kuunda kanisa la Wesley.

³⁴ Ndipo baada ya kuhesabiwa haki na utakaso, kukaja Pentekoste. Ndiposa Pentekoste, wengi walitoka kwa Methodist na kadhalika, na wakawa Pentekoste kwa sababu ilikuwa nuru kuu zaidi. Sasa Pentekoste imeunda dhehebu kama tu kila moja yao!

³⁵ Sasa, Biblia yasema hayo. . . Haya ni maneno makali, lakini nitayasoma toka kwa Biblia. Nanyi msikizeni daktari wenu, au ye yote yule, akisema hili, nami ni ndugu yenu nikifundisha toka kwa Maandiko. Biblia ililiita kanisa Katoliki “malaya, kahaba, k-a-h-a-b-a.” Na Yeye aliita makanisa Protestanti yaliyolifuata, mama. . . au hayo yalikuwa “makahaba wa mama huyu.” Na uhusiano uliokuwako, kanisa Katoliki liliunda kile kitu na kuwafanya watu waamini nuru liliyokuwa nayo wakati huo, au waliyokuwa nayo wakati huo. Walutheri walitenda jambo lile lile. Na Biblia ilisema kuwa yeye alikuwa mwanamke mkuu wa namna hivyo.

³⁶ Sasa, mwanamke wa aina hiyo ni nani? Ni mwanamke aishiye na kufanya uasherati. Na makanisa yanatenda uzinzi wa kiroho na—na watu. Ona? Wanafanya hivyo, wanafanya hivyo! Hapa kuna Biblia inayofundisha Haya, nao wanaunda baadhi ya kanuni za imani na kadhalika zisizohusika na Biblia. Na kwa . . . hii ni karibu miaka ishirini *na kitu* nimesimama papa hapa na kumuuliza mhudumu ye yote, wakati wo wote, aje na achukue . . . si vitabu vyenu, kanuni zenu za imani, bali aje na achukue Biblia (katika Nuru ya Biblia) na kuithibitisha kuwa si sahihi. Ona? Naam.

³⁷ Na kuhusu kuhitilafiana, wao husema “Kuhitilafiana!” Nimetoa kadiri ya mshahara wa miezi miwili kama mtu fulani atanionyesha hitilafu moja katika Biblia. Haimo. Mnadhani imo, lakini haimo. Kama Biblia inahitilafiana Yenyewe, haifai kabisa, huwezi kuiamini. Kila Neno limetiwa pumzi na Mungu na hamna kuhitilafiana katika Biblia.

³⁸ Sasa, kanisa Protestanti, katika mipango yake, (kulingana na Neno la Mungu) linahusiana kwa jambo lile lile na kanisa Katoliki.

³⁹ Sasa, sina neno dhidi ya Wakatoliki. Baadhi wa marafiki zangu wapendwa sana, wanaoketi mumu sasa, wamekuzwa na Wakatoliki. Hapa, usiku wa juzi, nilipotoa ujumbe mkali kwa Roho Mtakatifu, juu ya Protestanti na Katoliki, Wakatoliki walikuja papa hapa madhabahuni na kusalimiana nami kwa mikono. Wao ni wanadamu kama tu sisi.

⁴⁰ Huwezi kujadiliana na kasisi wa Katoliki, kwa sababu hawaamini Biblia hii kuwa ndiyo Neno lote; wao husema ni “kanisa,” tunasema ni “Biblia!”

⁴¹ Wakatoliki husema, “Sisi Wakatoliki huenda kanisani na kuabudu, ninyi Waprotestanti hukaa nyumbani na kusoma Biblia.”

⁴² Nilisema, “Naam, ninyi huenda kanisani na kuabudu, lakini, nini?” Hilo ndilo jambo linalofuata, ona.

⁴³ Sasa, lakini Mungu alisema Yeye alikuwa katika Neno Lake. Hili ni Neno Lake Mungu nami naliamini. Mimi ni mwabudu wa Biblia. Hiyo ndiyo sababu sikubaliani na Uprotestanti na—na mipango hii ya—ya kanisa, kwa sababu wao hufundisha vitu visivyo Neno la Mungu. Kwa hivyo siwezi kujizuia kutokukubaliana nao. Siwachukii; la, bwana, wao ni ndugu zangu. Nami sigombani nao, lakini sikubaliani nao kwa sababu yanipasa nichukue yale Mungu asemayo na kuacha kinginecho cho chote kiwe uongo. Ona?

⁴⁴ Na sasa huo ndio uhusiano ambao . . . Na sasa Biblia ilisema kuwa mwanamke huyu, lile kanisa Katoliki, ambalo lilipaswa kuitwa, katika Biblia, Ufunuo sura ya 17, “Kahaba, naye alikuwa mama wa makahaba.” Nasi twaona kuwa Biblia ilisema kuwa *mwanamke* huwakilisha “kanisa.” Kwa hivyo basi kama yeye

alikuwa na binti waliokuwa makahaba, haingekuwa wavulana; haina budi kuwa ni binti, hapana budi kuwa ni makanisa. Na Uprotestanti ulizaliwa na Ukatoliki.

⁴⁵ Na sasa mnyama anayefuata... Au, jambo linalofuata ni hili hapa:

Nini maana ya “ile sanamu ya mnyama”?

⁴⁶ Ni—ni swali linalopatana na hilo, na mtu aliyeuliza ana swali nzuri. Imekuwa sasa, kama... Biblia hufundisha dhahiri kuwa kanisa Katoliki ndilo yule—yule mnyama. Biblia ilisema kuwa *mnyama* maana yake ni “nguvu fulani.” Sivyoy? *Mnyama*, Biblia ilisema kuwa *mnyama* ilimaanisha “nguvu fulani.” Na huyo *mnyama* alikuwa ule “Jiji la Vatikani,” ile “Serikali ya kidini ya Katoliki.” Vema. Na, sasa, hizo zilikuwa nguvu za kanisa zilizokuwa mnyama yule.

⁴⁷ Basi kanisa Protestanti lilitoka kwa kanisa Katoliki, na kuungana na kupata nguvu kidogo, hiyo ilikuwa sanamu.

⁴⁸ Kama kitu fulani... Kama kitu fulani kilifanywa katika mfano wangu, ingekipasa kufanana nami. Kama kitu fulani kilifanywa katika sanamu ya kanisa hili, ingekipasa kufanana na kanisa hili.

⁴⁹ Kitu fulani kilifanywa, mnyama... kikafanywa sanamu ya mnyama huyu, ambayo ilikuwa Ulutheri, Umethodisti, Ubatisti, Upentekoste, Uholiness, makundi hayo yote yakaunda utaratibu na kufanya sanamu iliyofanana na mnyama. Ndiyo hiyo!

⁵⁰ Sasa, “Je, unasema basi, Ndugu Branham, Wakatoliki wote, Wamethodisti wote, na Wabatisti wote wata...?” Sikusema hivyo.

⁵¹ Kunao maelfu na maelfu na makumi elfu ya Wakristo waliozaliwa mara ya pili katika makanisa hayo. Lakini, katika madhehebu yao, wanajaribu kuwaelekeza kwa kanuni fulani za imani, nao hawatazistahimili. Ka—kanisa, linapounda dhehebu, linakuwa chini ya kanuni fulani za imani.

⁵² Nami sina kanuni za imani ila Biblia. Hii ndiyo Kanuni za imani ya Mungu, na Roho Mtakatifu ndiye Mfasiri wa hilo, na Yeye yualileta toka kwa nuru moja hadi nyingine. Injili ninayoihubiri siku hizi, kama nitaishi kuona miaka mingine mia, tukiweza, kungekuwa na Nuru zaidi. Daima huja kila wakati.

⁵³ Mlizioa kutumia gari la ng’ombe, baba wa babu yako, alipoenda kumwona mama katika motokaa muundo T. Lakini sasa karibu sote husafiri kwa eropleni. Ona, tunaendelea; sayansi, inaendelea; elimu inaendelea; Injili inaendelea. Na Biblia ilisema vingendelee, kasema, “Wataenda mbio huku na huko, na maarifa yataongezeka.” Kwa hivyo hicho ndicho kiunganisho. Hiyo ndiyo sababu kuna... .

⁵⁴ Madhehebu ya makanisa Protestanti ndiyo sanamu ya mnyama, kwa sababu yameunda madhehebu kama tu vile

Katoliki lilivyo. Na Mungu hakuumuru Kanisa Lake liunde dhehebu katika wakati wo wote, lakini kila mara amelilaani! Sasa, mwafahamu? Si watu, kanisa!

⁵⁵ Wanapojaribu kuleta watu chini ya nu—nuru ya... Hapa! Ingekuwaje kama watu wangelijaribu kukufanya wewe uende nyuma na kuanza kutumia gari la ng'ombe? Hungeistahimili, tunaishi katika wakati bora zaidi. Hivyo ndivyo ilivyo nyuma kule. Kama mtu fulani atajaribu kuniambia, "Ee, jambo pekee likupasalo kufanya ni *hivi, vile*." Ninaishi katika wakati mwingine! Mimi... Hiyo ndiyo shida ya wahudumu, kila mara wanatazama nyuma.

⁵⁶ Hapa! Mwanasayansi Mfaransa alisema, haipati miaka mia tatu iliyopita, "Kama mtu angeenda shoti kwa mwendo wa maili thelathini kwa saa, uvuto wa dunia ungemwondoa duniani. Maili thelathini kwa saa!" Vema, wadhani sayansi ingerejea kwa hilo siku hizi? Haiwezekani! La, bwana. Wanazo zikienda yapata maili mia tisa au elfu kwa saa. Hata hivyo... Au wakati mwingine katika roketi, ndiposa inafikia maili elfu moja na mia sita kwa saa. Na bado inamsogeza mbele!

⁵⁷ Sayansi imemsongeza mwanadamu mbele, mbele sana, mambo makuu kwa akili zake kuliko yale... (na hilo ndilo jambo pekee yeye alilo nalo, ni ule mti wa ujuzi), zaidi kuliko wahudumu walivyomchukua yeye na roho yake, ambayo haina kikomo. Lakini jambo ni hili. Sayansi haitazami nyuma kwa yale sayansi ilisema miaka michache iliyopita, sayansi inachukua yale waliyo nayo sasa na kuendelea mbele kwa jambo jingine.

⁵⁸ Lakini muulize mhubiri; "Vema, tutaona yale Moody alisema kuli husu, tutaona yale Wesley alisema kulihusu Hilo." Sijui yale wao waliyasema kulihusu, najua yale Mungu alisema kulihusu sasa! Ndilo hili nami bado natazamia yaliyo makuu zaidi! Naam. Hiyo ndiyo sababu...

⁵⁹ Biblia ilisema, "Roho tatu chafu zilitoka katika kinywa cha huyo mnyama." Je, mnajua hizo roho chafu zinafanana na nini? Vyura. Je mliwahi kutambua jinsi chura alivyo? Chura kila mara hutazama nyuma, yeye hata hatazami mbele kamwe; hutazama nyuma, kila mara nyuma, kutazama nyuma.

⁶⁰ Lakini wale wenye uhai wanne waliokuwa na vichwa mbalimbali vinne, katika Ezekieli, walikuwa wakitazama mbele na hawangerudi nyuma. Walikuwa wakienda mbele wakati wote. Kila mahali walipoenda, walikuwa wakienda moja kwa moja mbele. Mwaona tofauti?

⁶¹ Sasa, huo ndio uhusiano ambao Uprotestanti ulio nao na Ukatoliki

⁶² Kwa hivyo ninyi kila mara hushambulia Wakatoliki, lakini "nyungu haiwezi kuita birika 'nyeusi.'" Naam.

⁶³ Nauliza, "Wewe u Mkristo?"

64 “Nataka ufahamu mimi ni wa kanisa Batisti.” Naam. Hilo halihusiani nalo kwa cho chote kile zaidi ya kusema kuwa wewe u wa nje hapa kwa . . . shambani mahali fulani.

65 “Vema, mimi ni wa kanisa Katoliki.” Hilo bado halikufanyi Mkristo. Kuwa wa kanisa Batisti au Methodisti haikufanyi wewe Mkristo.

66 Kuna njia moja pekee kuwa Mkristo. Neno *Mkristo* maana yake ni kuwa “kama Kristo.” Nawe huwezi kufanya hilo, huwezi kufanya hivyo kwa nafsi yako mwenyewe, hakuna njia yo yote uwezayo kufanya hilo. Yakupasa ujisahau mwenyewe, ujifie mwenyewe, na uruhusu Kristo aingie na aishi Maisha ya Kristo ndani yako.

67 “Mtu asipo. . .” Haya ndiyo Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa kwa Roho na kwa maji hataingia kamwe katika Ufalme.” Haijalishi kama yeye ni Mkatoliki, Mmethodisti, Mbatisti, au ye yote yule, huna budi kubatizwa katika maji kwa ondoleo la dhambi zako na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, au umepotea. Hilo ni Neno ya Yesu Mwenyewe. Kwa hivyo sasa kama u Mmethodisti, na umepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu na umebatizwa katika maji, Yesu alisema utaingia Mbinguni, Kama wewe u Mkatoliki na umetenda mambo yale yale, utaingia Mbinguni.

68 Lakini kama unashikilia tu hizo kanuni za imani ya kanisa Katoliki, au Methodisti, au kanisa Batisti, ungali umepotea. Na hiyo ndiyo sababu tuna hali hii ulimwenguni, tuliyo nayo siku hizi, kwa sababu watu wako tu kama . . . Wao husema, “Hilo ni kinyume cha imani yangu.”

69 “Je, unaamini katika uponyaji wa Kiungu?”

70 “Hilo ni kinyume cha imani yangu.” Hilo ni kinyume cha kanisa lenu; kanuni za imani za kanisa lenu zimejitungia hilo, ona, huna budi kutenda yale kanisa lisemayo. Na halafu mnawashutumu Wakatoliki; wamefanya jambo lile lile. Na ndiyo mnyama na sanamu ya mnyama! Na Biblia husema “Ye yote aliyeipokea hangeingia Ufalme wa Mbinguni, lakini atatupwa ambapo mbwa na wachawi, na kadhalika, na atateswa kwa moto na viberiti (mbele za Malaika watakatifu nchini) milele na milele.

Toka kwayo, rafiki! Ukatatane na Mungu! Naam, bwana.

71 Na sasa hebu nipate hili, sasa, nasi tutayaondolea. . . Sasa, mtu fulani aliniuliza leo, nimeulizwa mara mbili tatu;

27. Ndugu Branham, unaponena kuhusu, “chapa ya myama,” je, huamini watachanja hesabu ile kichwani mwako, au kuchanja kitu fulani mkononi mwako? La, bwana. Usitazamie hilo kamwe.

72 Itakuwa ni ususiaji! Bila shaka! “Hakuna mtu angenunua wala kuuza isipokuwa awe ni wa muungano wa makanisa.” Hiyo

ni kweli. Sasa, itakuja kama muungano fulani, kuunganisha kitu kile, kukifanya muungano wa kidini. Shika Neno langu, hayako mbali! Na utayaona, yamekaribia karibu sana.

⁷³ Sababu ya kutokujua mambo haya, mko hapa nyumbani wakati wote. Nifuateni kule ng'ambo katika nchi hizi ambamo Ukatoliki una mamlaka, wakati mmoja, na mwone yale yanayotendeka. Ndugu, huwaambia yote yawapasayo kufanya na yasiowapasa kutenda.

⁷⁴ Na hapa Biblia yanena kuwa Marekani (tuliypata katika unabii) ilianza kama *mwana-kondoo*, “uhuru wa dini,” na moja kwa moja wakaunganisha mambo hayo pamoja, naye akanena kama joka na kutumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake, hiyo ni Marekani! Naam.

⁷⁵ Mhudumu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, rafiki yangu, alisema, “Ndugu Branham, Mungu hataachilia kamwe Marekani ianguke, kwa sababu ya msingi wa waanzilishi wake wa kale, msingi wake ni dini.”

⁷⁶ Nilisema, “Yeye aliwaachilia Wayahudi; wakaangukabili shaka, nao walikuwa na msimamo bora kuliko tuliokuwa nao.” Na hiyo ni kweli. Mungu hapendelei vizazi fulani vilivyopita; wewe utembe mstarini, la sivyoyote, haumo katika Ufalme, hivyo tu. Hakika! Hilo ni kali mno, lakini hilo ni zuri kwenu. Hilo lalingana na Maandiko. Nasi tuna . . . sisi . . .

⁷⁷ Shida ni kwamba siku hizi, baadhi yenu wazee mwajua hili, tuna Uinjilisti mwingi sana wa Hollywood. Naam. Huo umezidi na ghasia chungu nzima na kufanya yasiyofaa, na ulimbwelimbwe mwingi, na vinginevyo, na kujigamba, na mengineyo; na “Nani atakayesimama akampokee Kristo kama Mwokozi wake binafsi? Mungu akubariki, ndugu utaenda Mbinguni hivi sasa.” Huo ni uongo! Huo ni uongo!

⁷⁸ “Mtu asipozaliwa mara ya pili!” Na iwapo yeye amezaliwa mara ya pili, Baraka ile ile iliyomjia pale itamjia hapa. Na tumepitia hayo tena na tena, na kote Maandikoni katika juma lililopita. Na kutambua kuwa katika watu wa mashariki, Roho Mtakatifu alipowashukia Wayahudi, ambao walikuwa wa kimshariki, watu wa mashariki, Roho Mtakatifu aliwashukia kwa ishara kuu na madhihirisho. Biblia ilisema kutakuwa karibu—wakati ambapo hata hungeweza kuutambua . . . ni kama usiku au mchana. Ilikuwa kama siku yenye mawingu, na kuendelea hadi sehemu ya mwisho ya jioni. Ndiposa jua lingechomoza kwa dakika chache mwishoni mwa jioni. “Wakati wa jioni kutakuwako Nuru.” Sivyoyote? Vema, hao ni watu wa magharibi, Mataifa, wakimpokea Roho Mtakatifu yule yule ambaye Wayahudi walimpokea nyuma kule, kwa ishara ile ile na madhihirisho. Hiyo ni kweli.

⁷⁹ Na, bila shaka, walimwengu watakuia wewe “mshupavu, wa dini aliyerukwa na akili.” Biblia, Yesu alisema wangepanya

hilo. Ninyi mu watu wa kipekee, nanyi mu watu wasio wa kawaida kwa sababu ninyi ni tofauti sana.

⁸⁰ Nalitambua katika ujirani wangu nyumbani, watu kule, wata...Hata watoto wangu wadogo; tunajaribu kuwaweka wasafi na waishi kistahifu kama wawezaavyo kuwa, lakini unaweza kuona jirani wakiwabadilisha hao watoto. Ona? Wanawabadilisha.

⁸¹ Nami najua, nina njia ya kujua mambo (nanyi mwajua hilo, mmeiona katika mikutano), mwajua kuwa wachungaji wa mjini husema, “Vema, sasa Billy ni mtu mzuri, hatuna neno dhidi yake. Lakini mwaona, hilo ni kundi la watu wa tabaka nyingine mbali na sisi.” Mungu ashukuriwe! Hilo ni sawa. Mungu ashukuriwe! Hiyo ndiyo ile Chapa. Hiyo ndiyo chapa tunayonena habari zake.

⁸² Tazama usiku uliopita, Roho Mtakatifu alipotabiri, miaka mia tisa kabla Wayahudi kumpokea Roho Mtakatifu, na kumwaambia itakavyokuwa, “Yule Mtu mwenye kidau cha wino akiwa na kidau cha wino cha mwandishi alienda kati ya Yerusalemu na kutia alama katika vipaji vya nyuso zao.” Sivyoy? Alinena juu yake kabla kanisa halijahukumiwa na Mungu. Na Tito alizingira kuta za Yerusalemu, katika A.D. 96, na kuuteketeza huo mji. Na hakukuwa na jiwe moja lililosalia juu ya lingine, kulingana na unabii. Na, leo, kitu pekee kilichosalia cha hekalu ni ukuta wa kale ulioko pale ambapo walikusanya hayo mawe, na pamesuguliwa sana ambapo Wayahudi hulia na kuomboleza kwenye ule Ukuta wa Kuombolezea, kitu pekee kilichosalia cha hekalu lile. Na ule Uislamu wa Omar uko mahali papo hapo.

⁸³ Na Yesu alisema, kama ilivyonenwa na nabii Danieli, “Mtakapoliona chukizo la uharibifu limesimama katika patakatifu,” kisha Yeye aliyatilia mkazo, katika mibano duara: “*Asomaye na afahamu.*” Ona? Naam. Hayo ndiyo. Na Yeye alisema ni siku ngapi...ungepita wakati gani hata Mataifa wange...majira yangekatiliwa mbali. Wao wangekanyaga hizo kuta, kisha Mungu angewarudia Wayahudi. Na tumefikia wakati huo! Ndio hawa Wayahudi wakirudi nyumbani kwa maelfu, katika miaka michache iliyopita. Nanyi mwajua tulivyoyahubiri usiku uliopita, jinsi Maandiko kikamilifu...kama tu kusoma gazeti, na dhahiri zaidi kwa sababu mnapata fahamu zaidi Yake. Ndiyo...

⁸⁴ Lakini, walakini, ile Chapa iliyotiwa katika vichwa vyao haikuchanjwa, sivyoy? Ilikuwa ni nini? Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na ni chapa gani itakayokuwepo katika hizi siku za mwisho? Biblia ilisema, “Muhuri wa Mungu ulikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa watu katika siku za mwisho.” Sasa hakuna...Waefeso 4:30, “Wala msihuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata

siku ya ukombozi.” Biblia yanena. Na Waefeso 1:13 yasema jambo lile lile, mahali pengine pengi, kuwa “Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu.”

⁸⁵ Muhuri ni nini? Muhuri hauwezi kuwekwa kwenye kitu cho chote hadi kimekamilika. Walutheri hawakutiwa muhuri, majira ya wakati wa neema hayakuwa yamekamilika bado, walihubiri kuhesabiwa haki. Wamethodisti hawakutiwa muhuri, (ninafikia swali hapa, nasi tutalifikia ba—baadaye kidogo), hawakutiwa muhuri, kwa sababu hayakuwa yamekamilika. Lakini ubatizo wa Roho Mtakatifu ni ukamilisho wa kazi ya Mungu!

⁸⁶ Yeye alisema, “Kunao watatu washuhudia Mbinguni: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, na hawa watatu ni Mmoja.” Huwezi kuwa na Baba pasipo Mwana, na Mwana pasipo Roho Mtakatifu, wao ni Mmoja.

⁸⁷ Yeye alisema, “Kunao watatu wanaoshuhudia duniani: maji, Damu, Roho, nao si mmoja bali hupatana katika habari moja,” naam, “katika kutiwa muhuri kumoja kukamilifu.” Kuhesabiwa haki chini ya Luther, maji; utakaso kwa Damu.

⁸⁸ Kuhesabiwa haki kulikuwa Warumi 5:1 “Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa...Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Kuhesabiwa haki kwa imani!

⁸⁹ Utakaso kwa Damu, Waebrania 13:12 na 13, “Yesu naye, awatakaswa watu kwa Damu Yake Mwenyewe, aliteswa nje ya lango.”

⁹⁰ Luka 24:49, “Na tazama, nawaleta juu yenu ahadi ya Baba Yangu; lakini kaeni humu mjini Yerusalemu, hata mvikwe uwezo utokao juu.” Matendo 1:8 “Akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, Uyahudi, Samaria, na hata pande za mwisho za dunia.” Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa udumu hadi Yesu arudi tena! “Kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena, bali mtaniona mimi kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari; mkifanya yale—yale ninayofanya, mtayafanya pia.” Kwa Roho Wake, akitenda kazi kupitia kwa Kanisa! Yeye alisema, “Mtadhihakiwa.” Kasema, “Waliniita mimi Mwenye nyumba, *Beelzebuli*, “mkuu wa wapiga ramli,” kasema, “je, si zaidi watakavyowaita wale walio wa nyumbani Mwake sasa?” Kasema, “Heri ninyi watu watakapowanena kila neno juu yenu, furahini na kushangilia; kwa kuwa thawabu yenu ni kubwa mbinguni kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.”

⁹¹ Hayo ni Maandiko. Ndiyo hayo. Kwa hivyo, mwaona, yakupasa tu uwe Naye rafiki. Sasa yakupasa ujiamulie, wewe ni mtu huru kujiamulia.

⁹² Lakini huo ndio uhusiano kati ya kanisa Protestanti na kanisa Katoliki. Yote mawili pamoja, kulingana na Biblia...

hao wanaoshikilia tu kanisa; si Yesu, sasa, kanisa. Watu kanisani wanaoshikilia Yesu Kristo na kumwomba Mungu awafungulie njia na kuwafanya...kuwapa Nuru, hawa ndio watu waliookoka, sijali yeye ni wa kanisa gani. Naam. Lakini kama yeye anashikilia tu dhehebu lake, yeye amechukua ile chapa ya upotovu, ambayo inachukua mahali pa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kinyume! Na Katoliki na Protestanti wote, ni sawa, Biblia ilisema, “Yeye alikuwa kahaba, wao walikuwa makahaba (binti zake).” Je, hilo ni dhahiri sana? Vema.

28. Kwa hivyo Roho...Je, Roho Mtakatifu bado yuatolewa kwa kuwekewa mikono? Wanafunzi walifanya hili, Petro, Paulo, na wengineo, je ingali yawezekana? Paulo aliipokea kwa njia hii.

⁹³ Naam, ndugu mpendwa, dada, ye yote yule aliyeandika kijikaratasi hi—hiki. Roho Mtakatifu bila shaka hupokewa kwa kuwekewa mikono.

⁹⁴ Sasa, watu wengi huniita mimi...kwa vile nimejulikana kama Mpentekoste, wakisema mimi ni Mpentekoste. Sijawahi kuwa mfuasi wa dhehebu la Pentekoste. Mimi ni huru kabisa toka kwa madhehebu yote, na kwa msaada wa Mungu ninakusudia kukaa hivyo kwa sababu naweza kusimama pengoni na kusema, “Sisi tu ndugu! Njoo hapa, tukashauriane.”

⁹⁵ Nalipoanza nyuma kule, kwa neema ya Mungu...Nanyi watu hapa, na makatibu wangu na wengineo wanaoketi hapa wajua, ningewasiliana na watu milioni kumi, au zaidi, ulimwenguni leo. Dhehebu jinsi gani lingeanzishwa! Ona? Naam. Lakini sitaki dhehebu, ni kinyume cha Biblia. Ninajaribu niwezavyo kuwafanya watu waokoke waliomo madhehebuni. Hilo ndilo jambo muhimu. Na ushawishi ule Bwana alionipa kwa watu, nitautumia kwa utukufu Wake badala ya kuuweka katika dhehebu fulani. Nitauweka kwa Yesu Kristo ambapo unapaswa kuwa. Hakuna dhehebu linaloweza kukuokoa; ni Damu ya Yesu Kristo tu.

⁹⁶ Lakini sasa, katika kuwekea mikono, sasa, nitatofautiana na...Sasa, ninyi Wapentekoste wapendwa, sasa msinikasirikie. Lakini sasa mfikiapo mahali pa kusema, “Tutaenda tukeshe kwa ajili ya Roho Mtakatifu,” hilo ni neno la namna gani linalotumiwa katika Pentekoste!

⁹⁷ Na nitasema hili kwa yale...si kudhuru dhamiri zenu. Msaada mkuu zaidi nilio nao hudumani ni wa Wapentekoste, kwa sababu wanaamini ujumbe wa uponyaji wa Kiungu na nguvu za Mungu. Wengine wote huyapuza.

⁹⁸ Lakini watu binafsi tu toka kanisani, waliochaguliwa asili kwa Uzima wa Milele, watakuja. Hivyo tu. Lakini wale ambao hawakuchaguliwa tangu awali, hawawezi kuja; na Mungu alisema hivyo, kasema, “Walichaguliwa tangu awali

kwa hukumu.” Yeye hapendi ye yote aangamie, bali, akiwa Mungu, Yeye aliona wangeushutumu Huo. Kwa hivyo hilo ni—ni hivyo tu, Yeye aliliona hapo kabla. Na hivyo ndivyo kule kujua tangu awali kwa Mungu kulivyo, kuona mambo hayo. Tena alitabiri ambavyo kanisa litakuwa limesimama hata katika siku ii hii. Na Mungu alijua haya tangu mwanzo. Kabla ulimwengu kuwekwa misingi, Yeye alijua kanisa litakuwa jinsi lilivyo siku hizi. Yeye alijua kabla ulimwengu kuwekwa misingi nitakuwa nimesimama hapa katika mimbara hii usiku huu. Yeye ni Mungu. Anajua mwisho tangu mwanzo.

⁹⁹ Sasa—sasa, Wapentekoste wamefundisha... Sasa, labda nitapata mashambulizi mengi kwa Hili, lakini yanipasa niwe mwaminifu kama yanipasa kuja kwa Neno. Hakuna jambo kama “kukeshi”! Mmekuwa katika kosa. Kukeshi hakumaanishi “kuomba,” *kukeshi* maana yake ni “kungoja.” Baada ya kule kupaa, baada ya Yesu Kristo... kusulubiwa, kule kutakaswa kwa mahali patakatifu. Na baada ya ile siku ya upatanisho, kule kufufuka... Ile siku ya upatanisho, Yeye alipouawa, ndiposa ni siku arobaini hadi kule kupaa, halafu Pentekoste. Lile neno *Pentekoste* maana yake ni “hamsini,” lilimaanisha siku hamsini baada ya lile toleo la upatanisho.

¹⁰⁰ Ndiposa baada ya toleo la upatanisho kutolewa, kila kitu kilikuwa kimekamiliwa, kimaandiko, kigeografia, kila kitu kama tu vile Mungu alisema. Na Pentekoste, ilikuwa wakati wa siku kuu, walipoleta malimbuko ya mavuno na wakawa na siku kuu.

¹⁰¹ Sasa, malimbuko ya—ya Kanisa, Kanisa la Roho Mtakatifu, lile Kanisa ambalo lilipaswa kudumu miaka elfu mbili hadi Yesu aje, malimbuko yalikuja katika Pentekoste. Ilikuwa siku kumi kabla wakati wa Pentekoste; ilikuwa siku arobaini baada ya kule kutakaswa, baada ya kutolewa dhabihu, hadi kupaa kwa Yesu Kristo. Yeye alisema, “Enendeni Yerusalemu mkangoje hata mtakapovikwa Uweza utokao Juu.” Matendo 1...

¹⁰² Matendo 2, “Hata ilipotimia Siku ya Pentekoste walikuwa katika moyo pamoja, mahali pamoja. Kukaja ghafula toka Mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.”

¹⁰³ Na ndipo ulimwengu wa kidini, nje kule, yale makanisa makuu ya kidesturi, yakaja na kuona watu hao wakipepesuka na kutenda kama watu walevi. Nao wakaja na kuwacheka na kuwafanyia mzaha, kasema, “Ona hili kundi la Wagalilaya! Wote wamelewa!” Waona kutoelewa kule?

¹⁰⁴ Na kwa rafiki yangu Mkatoliki, mbarikiwa bikira Mariamu alikuwa pamoja nao. Na kama Mungu hangemwacha aje Mbinguni pasipo kumpokea Roho Mtakatifu na kuwa hivyo, je,

wadhani utafika kule ukiwa umepungukiwa kwa lo lote, dada? La. Kwa hivyo tusijiinue, tujishushe.

¹⁰⁵ Usijali yo yote yale ulimwengu unayosema. Tazama yale Mungu anayosema! Hili ni Neno la Mungu. Yatupasa kulijenga kulingana na *hii* ramani, kwa sababu Yeye alimwambia Petro, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.” Kila kitu kingenecho kitatendeka. Iionyesha kuwa milango ya kuzimu ingelipinga, lakini haitalishinda. Na watu wanadhania wanaweza kulikomesha? Ungeweza kukomesha jua upesi zaidi. Hiyo ni kweli. Huwezi kulikomesha. Mungu ameliagiza liendeleo.

¹⁰⁶ Hapa, nilipoongoka kwanza, hata maskini mama yangu kule alidhani nimerukwa na akili. Mama mkwe wangu alisema, “Yeye yapasa apelekwe kwenye hospitali ya wenda wazimu.” Wahubiri mlini walisema, “Yeye atapoa hivi punde.” Nimekuwa nikiwaka wakati huu wote, bado—bado ninawaka, na bora zaidi wakati wote. Mbona? Siwezi kupoa, ni Mungu! Badala ya kupoa, umeenea ulimwenguni kote sasa.

¹⁰⁷ Jambo lile lile ambalo Yeye alisema nilipobatiza chini hapa kwenye Mto Ohio, wengi wenu walikuwa wamesimama pale, miaka ishirini na mitatu iliyopita, papo hapo kwenye Mto Ohio. Nuru ile, Malaika, alishuka akaja hata tulipokuwa na kusema, “Kama Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule kuja kwa kwanza kwa Yesu Kristo, Ujumbe wako utaleta Kuja kwa Pili kwa Yesu Kristo.” Na imetendeka. Ni . . . Yeye bado hajakuja, lakini ona yale umefanya, umeenea ulimwenguni, kote. Ona? Na siku hizi sasa, nikiwaza tu, zile — zile juhudi zilizofanywa, kumekuwa na mamilioni hakika.

¹⁰⁸ Hata gazeti la Katoliki litwalo *Mgeni wa Jumapili* lilinena juu yake, ya mamilioni walioingia ndani, kwa juhudi zile tu.

¹⁰⁹ Wengine husikia, nao husema, “Hilo ni Kweli! Niko tayari kuviacha hivi sasa, vitu hivi vya ulimwengu, niende nikahubiri Injili halisi.”

¹¹⁰ Hiyo ndiyo sababu wanatuita “Injili nzima,” wanafanyia mzaha Injili nzima. Lakini, ndugu, sitaki nusu ya cho chote, mimi. . . yapaswa iwe nzima kwangu. Kama sehemu yake ni nzuri, basi nyingine yote ni nzuri. Injili nzima!

¹¹¹ Sasa, ona, Roho Mtakatifu alirudi pale. Watu wa pentekoste walingoja, “Kukaja ghafula toka Mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.”

¹¹² Hakuna hata wakati mmoja waliwahi kungoja baada ya hayo. Petro alipokuwa akinena Maneno haya kwa Mataifa, Roho Mtakatifu aliwashukia, hata kabla hawajabatizwa. Sivyo? Alipo . . . Matendo 10: . . . 49

Petro alipokuwa akinena maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia... wote waliolisikia lile neno.

Na wale waliotahiriwa, ... walioamini, wakashangaa, watu wote wlaiokuja pamoja na Petro, kwa sababu... Mataifa... nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu.

Kwa maana walisikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu,

Ni nani awezaye kukataza maji, kwa kuwa hawa hawana budi... waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi hapo mwanzo?

Naye akazidi kukaa na kuwabati... akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. (naam; hakuna kungoja, hakuna kukesha) ...

¹¹³ Njia ya kimitume, Mungu hana utaratibu, moyo unapokuwa na njaa Yeye atakupa kile unachokionea njaa. Kama wataka Roho Mtakatifu, anaweza kukushukia sasa hivi.

¹¹⁴ Petro, aliposhuka akaenda kule kuhubiri, Petro alikuwa na zile funguo za Ufalme. (Nina swali la kufikia hayo katika dakika chache.) Yeye alikuwa na funguo za Ufalme. Yeye aliufungua katika nyumba ya Kornelio. Yeye aliufungua, kule kwa Wasamaria, akaufungua huku; lakini kumbuka kuwa Filipo alikuwa ameenda kule na kuhubiri kwao na kuwabatiza hao kwa Jina la Yesu Kristo, na Petro akashuka akaja kuwawekea hao mikono. Na, sasa, yeye alitenda jambo fulani kwa yule mchawi chini kule. Walikuwa na Simoni mchawi, kasema, “Nitakupa kiasi fulani cha pesa, unipe Kipawa hicho ili ye yote nitakayemwekea mikono yangu atampokea Roho Mtakatifu.” Sivyo? Kitu fulani kilitendeka! (Si baadhi ya hawa askofu wakuu walio na ukosi uliopinduliwa nyuma, wakija na kuwawekea mikono juu yao, kasema, “Nitawapeni baraka za kimitume.”) Kitu fulani kilitendeka Petro alipoweka mikono yake juu yao, na bado wangali wakifanya hivyo.

¹¹⁵ Nimewaona wao wakianguka kama inzi hivyo, Roho Mtakatifu awagusapo kwa kuwekewa mikono. Naam, hayo ndiyo ma—mafundisho ya kimitume ya kuwekeleana mikono. Mungu akubariki. Kama unatofautiana kidogo na hayo, niandikie tu kijikaratasi kesho usiku. Vema.

29. Kama theluthi mbili ya watu wa ulimwengu walisikia... bado wangali hawajasikia Injili, Neno la Injili, vipi... (Samahani. Limeandikwa kwa wino, nami nimekuwa nikitoka na jasho hapa na imeingia ndani yake. Hebu tuone)

¹¹⁶ [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]... ambaye amepokea Roho Mtakatifu sasa, na anahubiri kule Me—Mexico. Naye

alikuja nyumbani kwangu, akasema, “Ndugu Branham,” kasema “Je, wewe unashughulika na Wapentekoste?”

Nami nilisema, “Naam, bwana.”

Naye akasema, “Mimi ni Daktari Reedhead.”

Nikasema, “Nina furaha kukujua, karibu ndani?”

¹¹⁷ Yeye aliketi na kuniuliza jambo fulani. Kasema, “Nasikia kuwa uliwekewa mikono katika kanisa Batisti.”

¹¹⁸ Nilisema, “Naam.” Lakini nilisema, “Niliondoka humo,” nikasema, “kwa sababu singevumilia hilo, ni—ninaamini kuhubiri yale Biblia isemayo, si yale kanisa Batisti husema. Nami sina chuki na kanisa Batisti, hao ni wazuri tu kama kanisa lingine lo lote.” Nami nilisema, “Niliondoka humo ili niwe huru.”

Yeye akasema, “Vema, hakika, unajua kuwa sisi tu Wabatisti.”

Nami nilisema, “Naam, bwana.”

¹¹⁹ Naye alisema, “Nataka kukuuliza jambo fulani. Na ubatizo wa Roho Mtakatifu je?” Kasema, “Nimekuwa ndani na kuwaona hao wakipiga mateke viti na kuchapua miguu na kupaza sauti na kutenda yasiyofaa.”

¹²⁰ Nilisema, “Nimeyaona hayo yote, pia.” Lakini nikasema, “Ndugu nyuma ya hayo yote, kuna kitu halisi kabisa cha ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

¹²¹ Naye akasema, “Ndugu Branham, naweza kumpokea?” Yeye akasema, “Nina shahada nyingi sana!” Kasema, “Mimi ni Daktari, mimi ni *hiki*, nina shahada ya elimu ya juu zaidi, nina shahada yangu ya chuoni ya kwanza, nina kila aina ya shahada na shahada za heshima toka kote matafani na vitu kama hivyo,” kasema, “na Yesu Kristo yuko wapi?”

¹²² Nikasema, “Vema, Ndugu, Yeye yuko humu chumbani.”

¹²³ Yeye alisema, “Nilisimama na kuongea na Mwislamu imara, aliyeelimishwa Amerika, nami nilisema, ‘Mwache nabii wako mfu wa kale ukampokee Bwana Yesu aliyefufuka.’ Yeye akasema, ‘Kwa hisani yako, bwana, Bwana wako Yesu aliyefufuka aweza kunifanyia nini kuliko Mohammed wangu awezavyo?’ Kasema, Wote wawili waliandika Ma-Biblia, twaamini hilo.’ Kasema, ‘Wote wawili walikufa.’ Na kasema, ‘Na wote wawili walituhadi Uzima baada ya mauti, nasi tunaamini hiyo.’

¹²⁴ Yeye alisema, “Ee, lakini, waona,” yeye kasema, “sisi Wakristo tuna furaha.”

¹²⁵ “Kasema ‘Hata nasi.’ Kasema, ‘Naweza kutoa elimu ya mawazo kadiri uwezavyo.’ Na hiyo ni kweli. “Yeye alisema, ‘Vema, tazama Mohammed wetu. . . Mlidai Bwana Yesu wenu alifufuka toka kwa wafu.”

¹²⁶ Na Daktari Reedhead alisema, “‘Vema, Yeye alifufuka!’”

127 “Kasema, ‘Lithibitishe!’ Kasema, ‘Lithibitishe!’ Kasema, ‘Mmekuwa na miaka elfu mbili kulithibitisha, na yapata theluthi moja pekee ya ulimwengu ndiyo imelisikia.’ Kasema, ‘Hebu na Mohammed afufuke katika wafu na ulimwengu mzima utajua hayo katika siku mbili.’” Yeye yu sahihi. “Yeye alisema, ‘Mohammed wetu hakutuahidi lingine lo lote ila Uzima baada ya mauti.’ Yeye alisema, ‘Bwana wenu Yesu aliwaahidi nanyi waalimu kuwa mambo yale yale Yeye aliyofanya mngeyafanya pia.’ Na kasema, ‘Hebu tuone ninyi waalimu mkifanya hayo sasa, na’ kasema ‘tutaamini Yeye alifufuka katika wafu.’”

128 Yeye alisema, “Ndugu Branham, nilikwaruza mguu ardhini *hivyo* na kunena mengine.” Na shahada hizo zote! Mbona? Mungu ako wapi katika shahada hizo? Mungu hajulikani kwa shahada za Ph.D. na D.D. na L.D., na kadhalika.

129 Mungu anajulikana kwa imani rahisi, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo njia pekee. Mungu ndani yako, na Yeye hukufanya wewe “mwana wa Mungu,” hugeuza tabia yako. Na jambo lile lile, Mungu Muumba aliyevumba vitu vyote na kunena ulimwengu uwepo kwa Neno Lake, Roho yule yule ndani yako, hebu amini kila kitu asemacho Mungu na hakuna lo lote lisilowezezana. Kama waweza kuamini Hilo!

130 Hutasimama nyuma kwa kanuni moja ndogo ya imani na kusema, “Siamini, sikubaliani na hilo. Siwezi kuamini Mungu atafanya *hili*. Siwezi kuamini.” Unamwekea Mungu mipaka kwa kutokuamini kwako! Naam.

131 Kwa hivyo Dakatari Reedhead akasimama pale, naye akasema, “Ndugu Branham, mtu angeweza, hakika, kumpokea Roho Mtakatifu?”

132 Nilisema, “Naam, bwana, Daktari Reed, unaweza.”

133 Yeye alisema, “Kama Mungu, ajuaye moyo wangu, nami nakuamini wewe, nikijua wewe uko chini ya pumzi ya Mungu sasa hivi, nakutaka wewe u. . . Je, unaamini nakwambia kweli?”

Nikasema, “Najua wewe unasema kweli!”

Akasema, “Naweza kumpokea?”

Nikasema, “Piga magoti.”

134 Naye akapiga magoti kando ya meza zee ya kahawa. (Niliipata juu hapa, mtu huyo anaketi nyuma kule aliyeitengeza muda mfupi uliopita humu. Akiketi hapo, akavunja kioo kilichokuwa juu yake alipokuwa akipiga magoti. Yeye alisema, “Mungu, irehemu nafsi yangu iliyojaa dhambi.” Ndiposa nikaweka mikono juu yake, na ubatizo wa Roho Mtakatifu ukamjia papo hapo. Hivyo tu.

135 Naye ameliwasha hilo kanisa Batisti kila mahali sasa! Wao wote wako pale. Ndivyo. Naam, bwana.

136 Injili haiwezi. . . Yesu hawezi kuja hata. . .

137 Sikiza! Tumesambasa vitini ulimwenguni kote. Huwezi kwenda pembeni yo yote dogo ila kuna kitini kilichosambaswa, mtu fulani akipitia pale na theologia. Nenda ng'ambo siku hizi na ujiite "mmishenari," na uwatazame wakikuchekelea. Ingia India na useme, "Mimi ni mmishenari."

138 "Vema utatufundisha nini?" Wanajua sana kuhusu Biblia... Baadhi ya watoto wao kule wanajua kuliko baadhi ya waalimu hapa Amerika waijuavyo. Hata hivyo, ni kitabu cha mashariki. Na Kumbuka, wao walikuwa na Injili mamia na mamia na mamia ya miaka isijakuwepo Amerika. Mtakatifu Tomaso, lile kanisa kuu alilohubiria, bado lipo sasa katika India. Hawahitaji yo yote ya mafundisho yenu, wanajua yote. Wao husema. "Mtatufundisha sisi nini?"

"Vema, sisi tu wamishenari Waamerika."

139 "Mtatufundisha sisi nini, jinsi ya kunywa mvinyo? Hayo ndiyo ninyi nyote mfanyayo kule makanisani mwenu! Kuvuta sigara? Mnakuja kutufundisha jinsi ya kutaliki wake zetu, na kadhalika?" Kasema, "Kama mtafanya hayo, hatuyataki." Na kasema, "Mtakuja hapa na theologia mpya au kitu fulani kile, mtajaribu kutufundisha baadhi ya Neno, twajua mengi zaidi kulihusu kuliko mfanyavyo ninyi." Na hiyo ni kweli. Yeye alisema, "Lakini kama mnakuja kudhihirisha Neno lisemavyo, tutalipokea." Amina! Naam. Hilo ndilo jambo wanalolitamani sana.

140 Shikeni Neno langu, liandikeni katika kurasa za Biblia zenu, maana ni BWANA ASEMA HIVI, "Kumbukeni, tufikapo India, mtasikia juu ya makumi ya maelfu mara elfu wakiokoka." Roho Mtakatifu amesema Hilo, nimeliandika hapa katika Biblia yangu. Limeandikwa katika makumi ya maelfu ya Biblia papa hapa, kama kule kufufuka kwa yule mvulana mdogo. Kwa ono ambalo Yeye alisema, "Kunao elfu, mia tatu ndani kule." Na mtaona kama hilo si sahihi! Hivyo ndivyo Injili itakavyohubiriwa kwa muda mdogo sana. Itaenea hivyo toka mahali hadi mahali.

141 Katika Afrika, ambapo hao elfu thelathini katika wito wa madhabahuni mmoja pekee, walimpokea Mungu, nilisema, "Inueni mikononi yenu mkampokee Roho Mtakatifu." Nilisema, "Msingojee baadhi ya wamishenari Waamerika waje hapa na kuwafundisha kunena lugha makanisani." Na akina mama wakisafishia juu ya mbao wampeleke mmishenari kule; na kuendesha motokaa nzuri kubwa, akiishi kwa vinono vya nchi; naam, asambase vitini vichache na kurudi. Hawataki hayo; imethibitika.

142 Nilisema papa hapa kwenye Hospitali ya Wayahudi pale, usiku mchache uliopita nilipokutana na wahudumu pamoja na madaktari, juu ya uponyaji wa Kiungu, nilisema, "Mliniita mimi mtakatifu anayejigaragaza, na kusema nilikuwa na

jinamizi nilipokuelezeni kuhusu yule Malaika wa Bwana.” Nami nilisema, “Na kanisa letu wenyewe limetuma maelfu na kutumia mamilioni ya dolla, kuwatuma wamishenari Afrika na nilipoendapo kule, walikuwa wakibeba sanamu ndogo za udongo, wakijaribu kupata msaada toka kwa sanamu za udongo, na wajiita wenyewe Wakristo.” Nami nilisema, “Kile mnachokiita ‘ushupavu wa dini’ kilileta nafsi nyingi zaidi kwa Kristo katika muda wa dakika tano kuliko yale mamilioni yetu ya dolla na maelfu ya wamishenari waliyofanya katika miaka mia na hamsini iliyopita.” Walinyamaza kimya, ndivyo ilivyo! Ndiyo hiyo pale. Nami nilisema, “Je, si ninyi. . .” Kwao watu, nikasema, “Msi—msijaribu kujielimisha, chukueni tu Injili hii na muende kule katika—katika nchi ya wenyeji ambapo hata mtu mweupe hawezi kuenda, kwa ajili ya magonjwa.

¹⁴³ Nami nina ushuhuda, toka kwa magazeti ya kule Durban, yalisema, “Hata huyo mzee mmoja asiyejua mkono wa kuume wala wa kushoto, alipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, naye alikuwa akibatiza wastani wa watu elfu moja kwa juma.” Hivyo ndivyo Injili inavyoendelea, kidogo tu, inahitaji tu yapata miezi sita hivi kuenea ulimwengu kote. Vema.

30. Tafadhali eleza kuhusu Christian—Christian Science?

¹⁴⁴ Vema. Mimi. . . Kuna. . . Sitasema kuhusu dini yako, ndugu yangu au dada, ye yote aliyeuliza swali hili. Christian Science ni elimu ya kimawazo. (Na uponyaji wa Kiungu ni nguvu za Mungu!) Christian Science ina nia juu vitu; Christian Science hukataa Damu ya Yesu Kristo. Christian Science. . . La, nina vitabu vya Bi. Eddy juu pale, nami nimwevisoma vyote. Ona? Naam, Christian Science hukana Ungu wa Yesu Kristo, na kumnena kuwa “nabii.” Yesu Kristo hakuwa mwanadamu, Yeye alikuwa Mungu! Yeye alikuwa wa Kiungu! Nao hudhani ni nia juu ya vitu.

¹⁴⁵ Kama nina kiharusi mkononi mwangu au tumboni, au katika. . . au maumivu kichwani mwangu, nina ujuzi kutosha kujua inaumiza, na si kama ninadhani inaumiza. Lakini najua kuwa nguvu za Mungu zaweza kuyaondoa, si. . . mimi kuwaza kuhusu hilo. Ona? Kwa hivyo Christian Science (nitasema hili pamoja na lile lingine nililoulizwa) ni mojawapo wa dhehebu mamboleo, na lililo katika kosa kuu kabisa. Naam. Si kuumiza dhamiri yako, rafiki, ye yote yule uliyeliandika, lakini lazima niwe mwaminifu. Kwa sababu wewe uliyeliandika, nami, pamoja, siku moja tutasimama katika Uwepo wa Yesu Kristo kutoa hesabu, nami yanipasa nitoe hesabu kwa yale ninayosema. Sasa, singelijibu nisingalijua. Naam.

31. Sasa, tunapo. . . Tunapoishi mbali na hapa. . . Wanasema: Sisi huishi mbali sana na hapa kuhudhuria maskani, unatushauri tuhudhurie wapi, tukutanike pamoja, kwa sababu makanisa yanafuata mama kahaba, au, Ukatoliki?

¹⁴⁶ Ndugu yangu mpendwa au dada, ye yote yule aliyeandika, singekuambia uhudhurie kanisa gani. Lakini lile ningefanya, ni hili, ndugu yangu au dada, mimi . . . Kama hujapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ona, vema, pokea ubatizo wa Roho Mtakatifu ndiposa uhudhurie kusanyiko lo lote ambapo mna watu wengine walio na ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Una . . . shiriki pamoja na watu wa namna hiyo!

¹⁴⁷ Nilimwona mtu hapa, si muda mrefu umepita, aliyezaliwa miaka kumi tangu . . . au, si kuzaliwa, samahani, ilikuwa miaka kumi tangu alipopata kuona cho chote. Yeye alikuwa wa kanisa kuu, naye aliishi kule Kennett, Missouri. Naye aliisha kuwa na . . . yeye alikuwa fu—fundi wa viatu miaka mingi iliyopita, na akawa kipofu. Na mtu huyo akaja jukwaani, na Roho Mtakatifu akamwambia yeye alikuwa nani na alipatwa na nini, kamwambia amekuwa kipofu kwa muda gani, kamwambia tendo fulani ndogo na chafu alilokuwa amefanya. Yeye akasema, “Mungu akiniruhusu niishi nifike kule nitarekebisha hilo.” Na, aliposema hayo, macho yake yakafunguka na Biblia ii hii, yeye aliisoma sura kwa sura.

¹⁴⁸ Yeye alirudi katika kanisa lake na alikuwa akishukuru. Naye mchungaji akamwambia, “Ingetendeka haidhuru. Naam, ulichochea tu, hamna kitu kwake. Upuzi huo haufai kitu, ni wa Shetani!”

¹⁴⁹ Namhimiza mtu ye yote anionyeshe Andiko moja ambapo Ibilisi anaweza kuponya. Ukinionyesha mimi ambapo Shetani aweza kuponya, nitakuthibitishia Shetani ni baba yako (na hiyo ni kweli) ukifanya hilo. Haliko katika Maneno ya Mungu. Haliwezi kuthibitishwa. Na huenda uka . . . unaweza kutaka kulijaribu, umekaribishwa. Lakini hilo limejaribiwa na maaskofu na wengine wote, ndugu, kwa hivyo usiseme hivyo.

¹⁵⁰ Tazama! Na mtu huyo alianza (moyoni mwake) kuliadini. Na miezi mitatu baadaye yeye alikuwa katika ibada zangu, kipofu tu kama alivyokuwa kwanza. Naam.

¹⁵¹ Kwa hivyo ondoka kwa hayo madhehebu! Kusanyikeni na watu wanaoamini, shiriki pamoja nao. Biblia ilisema, “Usijitie nira pamoja na wasioamini.” “Jitengeni,” asema Mungu. Ondokeni! Biblia ilisema “Ondokeni kati yao, na . . . usiguse kilicho kichafu, nami nitakupokea. Mimi ni Bwana nisimamaye katikati ya kanisa.” Naam. Ondokeni! Msishiriki na wa aina hiyo!

¹⁵² Lakini hebu . . . enda kwenye kanisa fulani, kanisa fulani nzuri. Methodisti, Batisti, Presbiteria, Campbellite, lo lote lile, haija . . . Walipo waamini halisi, hawajali kanuni za imani za kanisa zinasema nini, wanaenda kule kukutanika na ndugu zao na dada na kumwabudu Mungu, pamoja. Vema.

32. Usiku uliopita ulinena kuhusu “Umati mkuu ambao hakuna mtu angeuhesabu, toka kila kabila, taifa,”

ambao—wametajwa katika mlango wa 7 wa Ufunuo. Je, nilikufahamu, vyema, ukisema kuwa “Hao ni Bibi-arusi wa Kristo?” Naam, ulinifahamu, hao ni Bibi-arusi

¹⁵³ Sasa ukichunguza, hasa katika Ufunuo 7, yeye aliona mia na arobaini na nne elfu. Sasa, sikulaumu kwa hili, ndugu yangu, lakini wale mia . . . Kwa kawaida ni Shahidi wa Yehova ndiye aminiye kuwa hao mia na arobaini na nne elfu watakuwa Bibi-arusi. Na hilo ni kosa! Yohana aliwajua kila mmoja wao, naye akataja majina yao. Kila mmoja wao alikuwa Myahudi. Yeye alisema, “Kumi na mbili elfu, ni Gadi, kumi na mbili elfu, ni Zabulon; kumi na mbili elfu, ni Benjamini; kumi na mbili elfu ni Yuda.” Sivyo? Na kuna makabila kumi na mawili ya Israeli, na kumi na mbili mara kumi na mbili . . . ni mia na arobaini na nne elfu. Sivyo? Yeye alisema, “Na wote walikuwa wana wa Israeli.” Yohana aliwatambua.

¹⁵⁴ Ndipo yeye akatazama *huku*, naye akasema, “Naam, hapa kukasimama umati ambao hakuna mtu angewahesabu, wa makabila yote, lugha, na mataifa; walisimama wamevikwa mavazi meupe, mikononi mwao . . . na mitende, huku wakiipeperusha, na kupiga shangwe, na kuimba hosana na . . . kwa Mfalme.” Akasema, “Hao ni akina nani?”

¹⁵⁵ Yeye alisema, “Hao ndio wanaotoka katika ile dhiki iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao katika Damu ya Mwana-Kondoo. Wao wako mble za Mungu, nao watamtumikia Mwana-Kondoo katika Hekalu Lake pamoja Naye. Mchana na usiku, hawatamuacha Yeye.” Huyo ndiye Bibi-arusi, ona, yule Mke, Bibi-arusi Mtaifa.

¹⁵⁶ Kumbuka, Bibi-arusi ni Mtaifa. Yeye alisema, “Yeye atakuja na kuwatwaa watu toka kwa Mataifa kwa ajili ya” (kwa ajili gani?) kwa “ajili ya Jina Lake.”

¹⁵⁷ Sasa, kuna wasichana we—wengi ulimwenguni. Lakini nimemchukua mwanamke mmoja, na huyo alikuwa Meda Broy, na yeye ni Bi. William Branham sasa. Yeye ana . . . Yeye si Broy tena, yeye ni Branham sasa. Ona?

¹⁵⁸ Na hivyo ndivyo ilivyo, unampokea Yesu Kristo na ukuwa Bibi-arusi, washiriki wa Bibi-arusi.

33. Ni maneno gani ya Kilatini yaliyoko juu ya Jiji la Vatikani? Tunataka tujue jinsi yanavyojumulishwa kuwa mia sita na sitini na sita, na maana yake.

¹⁵⁹ Vema, hayoko juu ya . . . maneno yale ya Kilatini—yale ya Kilatini hayamo juu aya Jiji la Vatikani, yako juu a ya kile kiti cha enzi cha papa ambapo yeye hukalia kwenye kiti chake cha enzi. Imeandikwa juu pale, “VICARIVS FILII DEI” Mkitaka, asubuhi, nitayaleta yameandikwa, kila kitu, yameandikwa kwenye kipande cha karatasi. Na mkitaka, naam, nitawaletea ninyi asubuhi. Ambapo mnaweza kuyaendeleza katika herufi za Kirumi, VICARIVS FILII DEI, maneno haya maana yake ni

“Badala ya Mwana wa Mungu; yeye ni halifa wa Mwana wa Mungu.”

¹⁶⁰ Kanisa Katoliki huamini kuwa “Petro alikuwa papa wa kwanza, eti alikuwa halifa wa Yesu Kristo.” Ambalo hilo ni kosa! Vema. Ndipo wao hudai kuwa “Kila papa anayemfuata ni halifa; na papa sasa, aliyeko sasa, ni halifa wa Yesu Kristo.” Na yameandikwa juu pale, *Halifa wa Yesu Kristo*, “VICARIVS FILII DEI” imeandikwa pale. Chukua herufi za Kirumi ukaziandike tu (X ni kumi, V ni tano, na kuendelea hivyo), unapoendeleza herufi za VICARIVS FILII DEI,” chora mstari, na utapata mia sita na sitini na sita. Ziandike utaona.

¹⁶¹ Sasa, nina kile kitabu kiitwacho *Mambo Muhimu ya Imani Yetu*, kinavyoitwa, katika kanisa Katoliki, kwa sababu watu wangu ni Wakatoliki Wa-Irish. Kwa hivyo najua ninalonena. Ona?

¹⁶² Na hakika ni kweli kabisa, naam, kuwa kuna... Na Biblia ilisema kuwa “Yeye atakuwa ameketi katika kanisa, au mamahali fulani, au yataenea ulimwenguni kote. Naye anaitwa mpinga Kristo.”

¹⁶³ Na toka kanisani mle yanatokea makanisa madogo yaliyozaliwa baada ya hilo na kasema, “Yeye alikuwa kahaba, nao walikuwa makahaba walioandamna naye.” Hiyo ni kweli. Ndivyo ilivyo. Kwa sababu waliunda dhehebu katika kitu kile kile, na walikuwa na kanuni za imani zao na mafundisho. Yamepungua tu kidogo, hayana mamlaka kama lilivyo, lakini bado wana nguvu. Na *mnyama* maana yake ni “nguvu.” Naam. Kwa hivyo wao wana... Katoliki ina nguvu kuu zaidi. Methodisti, ndipo kulikuwa na Wapresbiteria, kisha Walutheri, kisha Wabaptisti, na nyinginezo, na kadhalika. Hizo zilikuwa nguvu ndogo, zilizounda dhehebu, “Kanisa langu! Kanisa langu! Kanisa langu! Kanisa Langu!”

¹⁶⁴ Lakini mwamini wa kweli hasemi lo lote kuhusu hilo, ni “Kristo wangu! Kristo wangu! Kristo wangu!” Hiyo ndiyo tofauti, mwaona. Unajuaje? Roho Mtakatifu anashuhudia kwa ishara na maajabu.

¹⁶⁵ Hapa kunalo dogo, aina fulani ya kuvurumishwa nyuma. Nachukia kusoma hili, lakini mtu fulani aliliweka juu hapa;

34. Uliuliza sababu gani Maskani haya hayaendelei. Sababu ni kuwa, ni kwa sababu mashemasi fulani hukana karama za lugha na uponyaji. Sisi sote twajua hilo kuwa kweli.

¹⁶⁶ Hebu nijue yeye ni nani, hali niko hapa kwenye hii—kwenye hii kampeni, na huyo ataondolewa upesi. Mwaona? Ona?

35. Tafadhali eleza kama Mkristo apaswa kuadhimisha kutawadha miguu na ubatizo kwa Jina la Yesu Kristo (Jina) badala ya jina la “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” Tafadhali.

167 Vema. Nilikuwa na karibu matatu ya hayo ndani humu yaliyouliza jambo lile lile.

168 Kutawadha miguu, vema, heri nianzie kwa hilo. Vema, sasa huenda akatofautiana, hilo ni sawa. Hebu nisome machache, kwa muda mchache. Au ukitaka kuyasoma fungua Yohana Mt., mlango wa 13, kwa muda mchache. Nataka kuwaulizeni kitu fulani hapa. Basi sikiza yale Yesu Kristo alisema, Mwenyewe, ndiposa nitawapeleka katika Agano na kuwaonyesha yangali yanaadhimishwa. Anzia kifungu cha 2:

Hata wakati wa chakula cha jioni naye ibilisi amekwisha...kumtia Yuda, mwana wa Simoni Iskariote, moyo wa kumsaliti;

Yesu hali akikua...ya kuwa baba amempa vyote mkononi mwake,...naye kuwa alitoka kwa Mungu (Yeye alitoka kwa Roho, akaingia mwilini, na akarudi tena katika Roho. Ona?)

Aliondoka chakulani; akaweka kando mavazi yake... akatwaa kitambaa,...akajifunga kiunoni.

Kisha akatia maji katika bakuli, akaanza kuwatawadha wanafunzi miguu, na kuifuta kwa kile kitambaa alichojifunga.

Hivyo yuaja kwa Simoni Petro. Huyu akamwambia, Bwana! Wewe wanitawadha miguu mimi?

Yesu...akajibu, akamwambia, ni—nifanyalo wewe hujui sasa;...lakini utalifahamu baadaye.

Petro akamwambia, wewe hutanitawadha miguu kamwe. Yesu akamwambia, kama nisipokutawadha, huna shirika nami. (Ee, waweza kuwaza hilo! Vema).

Simoni...akamwambia,...Bwana, si miguu yangu tu, hata...mikono yangu na kichwa changu pia.

Yesu akamwambia, Yeye aliyekwisha kuoga...hana haja ila...ya kutawadha miguu, bali yu safi, mwili wote; nanyi mmekuwa safi,...lakini si nyote.

Kwa maana alimjua yeye atakayemsaliti, ndiye maana alisema, Si nyote mko safi.

Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na — na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena, akawaambia, Je! mmelewa na hayo niliyowatendea?

Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo.

Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu,...imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi.

Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.

... *mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyajua mambo haya*
na kutenda haya.

¹⁶⁹ Katika 2 Timotheo, Paulo alisema, akiandikia kanisa, “Msimkubalie mjane aingizwe kanisani hadi yeye amewaosha watakatifu miguu.” Hiyo ni kweli. Kutawadha miguu kuliadhimishwa kote katika siku za Biblia. Na kwa msaada wa Mungu nikiwaza vema, na Mungu akinisaidia, nitakuadhimisha hadi nife. Naam. Ni agizo la Yesu Kristo hasa!

Sasa, hapa kuna swali litakalochoma:

36. Je, kwa nini mtu abatizwe katika Jina la Yesu Kristo badala ya “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu”?

Ninayo mawili matatu hapa, hapa kuna moja papa hapa:

37. Ndugu Bill, ni ubatizo upi wa uongo uliokuwa ukiunena usiku uliopita, kama ni wa maji au wa Roho? Kama ni wa maji, nawe ulisema Jina la Yesu Kristo, mbona Mathayo 28:19... inasema “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?” Tafadhali eleza.

¹⁷⁰ Sasa, haya yanachoma-choma, lakini naamini nina lingine hapa mahali fulani, [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] Kama mahali patatu. Nitajaribu kulifikia. Hebu tuone. Je, mnaweza kunistahimili kwa dakika chache? Vema. Sasa, hebu tuanze sasa kuyajibu maswali haya. Labda tunaweza kuruka baadhi yao, na labda kuyapata (yaliyosalia) kesho, kama hamna kitu kwa ajili ya shule ya Jumapili, au wakati mwingine. Lakini watu hawa, jamaa, wanauliza hili, na kesho ni ubatizo. Sasa, kwa njia ya yote uliyobatizwa, ni mambo kwangu. Lakini nataka — nataka kukwambia Mafundisho ya kimitume ya Biblia. Ona?

¹⁷¹ Sasa, tuliona, usiku uliopita, kuwa kanisa Katoliki lilipounda dhehebu, kwamba lilibuni uishirika wa uongo, kasema kuwa “Unapopokea Ukaristi takatifu, wakimaanisha ushirika mtakatifu, unampokea Roho Mtakatifu.” Hiyo si Roho Mtakatifu, huo ni mkate mwembamba.

¹⁷² Kanisa Protestanti husalimiana kwa mikono, huweka majina yao kwenye kitabu, hiyo ndiyo wanayoita “kumpokea.”

¹⁷³ Sasa, lakini njia halisi ya kumpokea ilikuwa ubatizo wa Roho.

¹⁷⁴ Na, sasa, kanisa Katoliki lilileta katekismu. Luther alikuwa nayo, kanisa Methodisti linayo, Wa-Episcopalia wanayo. wengine wengi wanayo, katekismu. Mapokeo mengi ya kanisa Katoliki bado yamening’inia kwenye kanisa Protestanti; ambalo lina haki zake kwake, kulingana na Biblia.

¹⁷⁵ Lakini hamna mtu (kamwe), katika kurasa sote za Biblia, aliyebatizwa kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Hamna mtu aliyebatizwa kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Makatifu” hadi kanisa Katoliki la mwanzoni. Haimo katika Biblia, hamna po pote! Na kama mtu ye yote aweza kupata

sehemu ndani mle, na aniambie na kunionyesha ambapo mtu mmoja alibatizwa kwa kutumia jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” tafadhali anionyeshe, kwa maana nimechunguza kote na kote, na kote na kote na kote humo; kwa miaka ishirini na kitu sasa. Na ni kosa! Ni kanuni ya imani ya Katoliki na si agizo la Biblia!

¹⁷⁶ Sasa tutatambua sababu yake, tunaandea swali lako hapa, ndugu... Yohana Mt... Nakusudia Mathayo 28:19. Vema, hebu turudi nyuma. Fungueni Biblia zenu pamoja nami, ili mkasome nami. Hapa ni mahali ambapo imenenwa. Mahali pamoja katika Biblia ambapo...

¹⁷⁷ Je, Yesu hakusema, “Kwa vinywa vya mashahidi wawili watatu kila neno lithibitike?”

¹⁷⁸ Naweza kukupeleka katika Biblia ambapo ilisema, “Yuda Iskariote alienda akajinyonga,” na, “Nenda katende vivyo hivyo.”

¹⁷⁹ Naweza kukupeleka ambapo Yesu alisema, “Mwana wa Adamu” (ambaye alikuwa Yeye Mwenyewe) “aliye sasa Mbinguni atakaporudi tena,” na huku amesimama papa hapa duniani. Na kasema, “Mwana wa Adamu aliye sasa Mbinguni sasa,” na huku amesimama papa hapa duniani.

¹⁸⁰ Yakupasa umjue Mungu kujua Neno Lake. Huwezi... Si ajabu unasema, “Inahitilafiana Yenyewe. Ni mchafuko.” Kwa maana Mungu alisema Yeye aliandika hivyo kuificha kwa hawa wanavyuoni na kadhalika. Na hebu watu wanyenyekee madhabahuni, na Mungu atakufunulieni.

¹⁸¹ Sasa ndilo hili Andiko, Mathayo 28:19, mahali pekee katika Biblia palipowahi kutajwa vyeo hivi.

Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu;

¹⁸² Sasa, jinsi unavyobatizwa ni “Kwa jina la Baba, na kwa jina la Mwana, na kwa jina la Roho Mtakatifu.” Hayo hata hayako katika Maandiko! Lakini ndiyo haya, “Mkiwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa Jina!” Sasa tazama kwenye Biblia yako uone kama hayo yanasema “kwa majina” au “kwa Jina.”

¹⁸³ Sasa, unasema... Sasa, hapa muda mchache uliopita mkutanoni, mtu fulani alisema, “Kuna hitilafu katika Biblia!” Kasema, “Laiti ungelinieleza. Mbona Yesu aliwaambia watu wabatize kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, na Petro akageuka na kuwabatiza wao katika Jina la ‘Yesu Kristo,’ katika Matendo 2: 38?” Kasema, “Kama hilo halihitilafiani, sioni hitilafu!”

Nikasema, “Kwa sababu tu hujamtafuta Mungu sahihi.”

184 Yeye akasema, “Ndugu Branham, je, kuna tofauti yo yote nikibatiza *hivi* au *vile*?” Bila shaka kuna tofauti, nami nitaithibitisha kwa Biblia.

185 Vipi kama—vipi kama Musa... Mungu alimwambia Musa, akisimama karibu na kijiti kile, kasema, “Musa, toa viatu vyako, umesimama mahali patakatifu.”

186 Yeye aseme, “Sasa, Bwana, mimi ni mstahivu. Ni shida kidogo kuvua viatu vyangu, kwa hivyo nitavua tu kofia yangu.” Yeye hakusema kwamwe “kofia,” alisema “viatu!” Na yale Biblia isemayo ni Kweli. Sasa kama...

187 Hapa, zimetimia siku kumi, huku ni kule kupaa. Na Yesu alipopaa, Yeye aliwaagiza wanafunzi Wake waende ulimwenguni kote na kuwafanya mataifa yote wanafunzi Wake, wakiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Na siku kumi baadaye... walienda Yerusalemu na kungoja orofani mpaka Roho Mtakatifu alipokuja. Ndiposa walipoanza kuhubiri na kuendelea... Wao walisema, “Tutendeje tuokoke?”

188 Petro akasema, “Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo.”

189 Kisha akaenda kwa nyumba ya Kornelio, naye akasema, “Tubuni mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo.”

190 Yeye alienda kule na kukuta watu fulani ambao walikuwa wamekwisha batizwa, kasema, “Yampasa mbatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo!”

191 Na akaenda Samaria na kusema, “Wabatize kwa Jina la Yesu Kristo.”

192 Na hakuna hata wakati mmoja vyeo hivyo vilipata kutumiwa kwa mtu. Hapana! “Sasa kuna hitilafu basi,” mnasema. La, sivyo. Muulize Roho Mtakatifu sasa na mtazame Yeye akikufunulia. Fungua moyo wako.

193 Sasa, usiwe na udhuru; ukifanya hivyo, Mungu hawezi kuongea nawe. Lakini bila udhuru, sema “Natafuta ukweli hasa, Ndugu Branham.”

194 Kama Yesu aliwaambia wanafunzi, “enendeni mkafanye *hili*,” nao walienda na kutenda vinginevyo *hapa*, hata hivyo Mungu akaibariki, na kote Bibliani. Sasa, walifanya yale Yesu aliwaambia wasifanye? Kama walifanya, hawakutii, na Mungu hataheshimu kutokutii. Na kama yeye angelikuheshimu, angemheshimu Hawa na kukomesha jambo lote hapo mwanzo. Mungu asemapo jambo lo lote, Yeye apaswa kutimiza Neno Lake, Yeye ni mwenyezi. Kwa hivyo, basi Petro huenda alikosea...

195 “Lo,” kasema, “hayo ndiyo mitume walisema.” Mtu mmoja alisema, “Hayo ndiyo mitume walisema, nitafanya Yesu alivyosema Yesu.”

196 Vema, kama mitume walifanya yale Yesu aliwaambia wasifanye, nini basi? Na kama mitume walioiandika Biblia hii, Paulo aliyaandika haya yote, na Paulo ndiye aliyewafanya wabatizwe tena, na kama Paulo aliyaandika haya, sehemu kubwa zaidi ya hili Agano Jipya, basi ni Biblia aina gani mliyo nayo iliyoandikwa mnayojaribu kusoma?

197 Hebu tufanye hivi tu, tuwe wenye busara sana na tuone yale Neno lisemayo. Sasa, hili ni kwa ajili ya elimu, mpate kujua Neno la Mungu.

198 Sasa, kama Petro alibatiza katika Jina la Yesu Kristo baada ya Yesu kumwambia abatize kwa jina la “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” yeye alifanya kinyume cha yale Yesu alisema. Hilo ni kweli? Sasa, hapana budi mna kitu fulani pale. Sasa hebu na tuchunguze, na tumwulize Roho Mtakatifu atuonyeshe sisi. Sasa, kwanza, sasa hebu—hebu tuchukue Maandiko ya kwanza, Mathayo 28:19.

Basi, enendeni...mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, . . . Mwana, . . . na Roho Mtakatifu;

199 Tazama katika Biblia zenu na mwone kama hivyo ndivyo isemavyo “kwa majina ya baba, na mwana, na Roho Mtakatifu.” Inasema hivyo? La, Bwana. Ilisema, “kwa jina la Mwana, kwa jina la Roho Mtakatifu?” Ilisema, “katika Jina!” Sivo? Vema, “jina” ni umoja. Sivo? Vema, alitaka wabatize kwa jina gani, jina la Baba, au jina la Mwana, au jina la Roho Mtakatifu? Yeye alisema, “Kwa Jina!” Vema, kusema kweli, hamna jina hapo.

200 Baba wangapi walioko ndani humu, hebu tuone mikono yenu—mkono wako. Vema. Nani kati yenu anaitwa “Baba?” Baba si jina, baba ni “cheo.” Wana wangapi waliomo humu? Hakika, kila mwanamume, kila mtu wa kiume, wao ni wana. Vema, nani kati yenu anayeitwa “Mwana?” Si jina, ni cheo. Sivo? Si jina, ni cheo. Vema, nani kati yenu anaitwa “Mwanadamu?” Wanadamu wangapi wako humu? Ninyi nyote. Vema, nani kati yenu anaitwa “Mwanadamu” Hakuna kitu kama hicho; hivyo ndivyo ulivyo. Roho Mtakatifu si jina; hivyo nidvyo alivyo. Mimi ni mwanadamu. Kwa hivyo au Baba, Mwana, au Roho Mtakatifu si “jina,” hivyo ni vyeo vitatu vilivyo na Jina moja.

201 Sasa sikiza kwa makini. Nini . . . Tazama hapa. Nitachukua hili kidogo kama maelezo ya mtoto mchanga. Kama ulisema, vema, kama ulikuwa ukisoma ki—kitabu cha hadithi, na kilisema, “Yohana na Mariamu wakaishi raha mustarehe.” Nawe unashangaa basi, “Nani Yohana na Mariamu?” Vema, jinsi tu unavyoweza kujua Yohana na Mariamu ni akina nani, ni kurudi nyuma na kusoma mwanzo wa hadithi hiyo na kuisoma yote. Sivo?

²⁰² Vema, kama Yesu alisema hapa, “Wabatize kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” na Baba si jina, na Mwana si jina, na roho Mtakatifu si jina, nini, Mtu huyu ni nani? Tunataka kujua Yeye ni nani. Sasa jambo bora kufanya... Hiyo ni sura ya mwisho ya Mathayo, kifungu cha mwisho. Hebu turudi nyuma kwa mlango wa 1 wa Mathayo na kifungu cha kwanza, tunapoanza, kuona huyu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni nani. Sasa, nataka tu kufanya hili kwa ajili ya watoto, na ndipo watalipata pia.

²⁰³ Jambo la kwanza, ni kukunyosha wewe kwa “utatu” wako, baba, Mwana Roho Mtakatifu. Sasa, kwanza, hakuna hata mahali pamoja katika Biblia ambapo *utatu* umetajwa. Patafute ukanionyeshe mimi. Hamna kitu kama hicho. Ni kosa la Katoliki, nanyi Waprotestanti hulikubali. Tazama, sasa. *Hii* ni nini? Sasa, nilisema huyu ni Nani? Baba. *Huyu* ni Nani? Mwana. Na *huyu* ni Nani? [Kusanyiko linasema, “Roho Mtakatifu!”—Mh.] Sasa, Baba ni baba wa nani? Mwana. Sivyo? Sasa, *huyu* ni Baba wa Yesu. Usiwachanganyishe, sasa. *Huyo* hapa ni Baba, *huyu* hapa ni Mwana, na *huyu* ni Roho Mtakatifu. Sivyo? Sasa, watu huwanena, kuwa, “Watu watatu mbalimbali, Miungu mitatu mbalimbali, nafsi tatu mbalimbali.” Si ajabu Wayahudi hawawezi kulifahamu! Vema.

²⁰⁴ Mathayo, sura 1, inaanza na ukoo wa Yesu Kristo, “Ibrahimu akamzaa Isaka, Isaka akamzaa Yakobo,” na kuendelea, kuendelea hivyo hadi kufikia kifungu cha 18:

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa...

²⁰⁵ Liko hapa, kifungu cha 18;

Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa... (nifuatani katika Biblia zenu)...kuzaliwa kwake Mtu huyu Yesu Kristo kulikuwa hivi: Alipokuwa...Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu,... alionekana ana mimba kwa uweza wa Mungu, Baba. (Je, niliisoma sahihi? Inasemaje? [makutano wasema, “Roho Mtakatifu!”—Mh.] Alionekana ana mimba ya Nani? Nilidhani mtu fulani alisema Mtu huyu alikuwa Baba Yake? Biblia ilisema Mtu huyu alikuwa Baba Yake)... alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

²⁰⁶ Sasa una mtoto aina gani? Kama Yesu alivyosema dhahiri, Mungu alikuwa Baba Yake. Sivyo? Mungu ni Baba Yake! Vema Roho Mtakatifu anahusikanaje nayo basi? Kama Biblia ilisema Roho Mtakatifu ni Baba Yake, na Yesu alisema Mungu alikuwa Baba Yake (nanyi mlisema Mungu alikuwa Baba Yake, na sasa Biblia inasema hilo hapa), kama kuna watu—watu wawili mbalimbali, Mungu hakuhusika nayo, Roho Mtakatifu ni Baba Yake.

²⁰⁷ Sasa hebu tuisome zaidi kidogo:

...Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, hakuwa akitaka kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa kisiri.

Basi, tazama, alipokuwa akifikiri hayo...malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. (si Mungu Baba; ni Mungu Roho Mtakatifu!)

208 Mwaona ambapo wazo lenu la kiutatu lingeelekea? Lingemfanya Yesu mwana haramu. Bila shaka. Hilo ni kosa! Hamna Andiko kwa hilo. Sasa, huna budi kukubali kuwa Mungu Baba, kwamba Mungu Roho Mtakatifu, ni Mtu yule yule, au Yesu alikuwa na baba wawili mbalimbali. Sivyo? Hakika, ni kweli. Biblia ilisema, "Roho Mtakatifu alikuwa Baba Yake," na Biblia ilisema, "Mungu alikuwa Baba Yake." Sasa, nani kati yao ni Baba Yake? Roho Mtakatifu na Mungu ni Roho yule yule, ni Kitu kile kile.

...hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa anabii, akisema,

...bikira atachukua mimba,...atamzaa mwana, nao... (Huyu)

...nao watamwita jina lake YESU: maana, yeye ndiye atakayeweokoa watu wake na dhambi zao,

Na yote hayo yamekuwa, ili litimie neno...

...watamwita jina lake Imanueli, yaani, Mungu pamoja nasi.

209 Sasa, nani Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu? Je, Petro alikosea? Yeye alitenda yale Yesu alimwambia. Hivyo ni vyeo vitatu.

210 Mimi ni mhudumu, nami ni baba, nami ni "Padre," wanaliita (cheo), lakini kati ya hivyo hamna jina langu. Jina langu ni William Branham.

211 Yeye alikuwa Baba, alikuwa mwana, alikuwa Roho Mtakatifu. Mnajaribu kufanya Miungu mitatu, rafiki; si sahihi, ni kosa.

212 Kuna nyakati tatu zilizowafarakanisha wa kiutatu. Mungu, Baba, alikuwa Roho aliyenig'inia juu ya Israeli katika ile Nguzo ya Moto. Sivyo? Mungu alikuwa kule. Ndipo Mungu alifanyika mwili akakaa kwetu (sivyo?) katika Mwana. Sasa Yeye alijidhili hata akaja katika moyo wa mwanadamu, kwa Roho Mtakatifu.

213 Mungu ni kama kijiti cha kupimia cha futi tatu, au, kijiti cha kupimia cha futi tatu, naam. Inchi kumi na mbili za kwanza zilikuwa Mungu, Baba; inchi kumi na mbili za pili, Mwana, Mungu yule yule; inchi kumi na mbili za tatu zilikuwa Mungu Roho Mtakatifu, Mungu yule yule. Yesu alisema...

214 Mnasema, “Tuna Roho Mtakatifu ndani yetu.” Naam.

215 Lakini Yesu alisema, “Kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni Mimi tena. Bali mtaniona Mimi, kwa maana Mimi. . .” (“Mimi” ni kijina cha mtu) “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Roho Mtakatifu yuko wapi basi? “Sitawaacheni ninyi yatima, naja tena niwe pamoja nanyi.” Naam.

216 Unaona, mnaielewa vibaya. Ni Mungu mmoja katika nyakati tatu. Muda wa majira ya Ubaba, Uwana, na Roho Mtakatifu, ni Mungu yule yule. Na Yeye aliposema, “Enendeni, mkawabatize kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,” ilikuwa ni Yesu Kristo. Na hiyo ndivyo sababu tunabatiza kwa Jina la Yesu.

217 Sasa, tazama, hebu tupate mabatizo hapa. Wakati wa kwanza *ubatizo* ulipowahi kutajwa katika Agano Jipya, ilikuwa Yohana Mbatizaji. Sivyo? (Nitaliweka *hili* juu hapa.) Mwaona, yakupasa ulainishe Uungu wako kabla hujanyosha ubatizo. Huyu ni Yohana Mbatizaji, ubatizo wa kwanza.

218 Mara ya pili ubatizo uliponenwa, ilikuwa Matendo 2:38, ambapo walibatizwa kwa Jina la Yesu Kristo katika kanisa mpya. Mahali panapofuata ilikuwa nyumbani mwa Kornelio, au si. . . samahani, Wasamaria, Matendo 7:48 na 49. Na Matendo 10:49 ndipo yeye alipowabatiza wao katika nyumba ya Kornelio. Na mara nyingine ubatizo uliponenwa, na kutajwa majina yo yote au vyeo, ilikuwa katika Matendo 19:5.

219 Sasa, walipobatizwa Siku ya Pentekoste, walibatizwa (Matendo 2:38) kwa Jina Lake Yesu Kristo. Sivyo? Na iandike, ukaichunguze.

220 Inayofuata, Filipo alishuka akaenda siku mbili baadaye, na kuanza kuhubiria Wasamaria; na akawahubiri, na kuponya wagonjwa, na alikuwa na mkutano mkubwa chini kule, na akawabatiza kwa Jina la Bwana Yesu Kristo. Petro akashuka akaenda na kuweka mikono juu yao wote nao wakampokea Roho Mtakatifu.

221 Petro alipanda juu ya nyumba siku chache baadaye, alikuwa na njaa, naye akaona ono. Mungu akamtuma kwa Kornelio. Na Petro alipokuwa akisema Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia, nao wakaanza kunena kwa lugha na kuendelea kama walivyofanya mara ya kwanza. Petro akasema, “Hata hawajabatizwa bado. Kwa hivyo akawaamuru, kila mmoja wao, kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo.

222 Kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Paulo. . . (Nakusudia, wanafunzi wa Yohana hawakuwa wamebatizwa kwa Jina la Yesu Kristo, walikuwa wamebatizwa tu ubatizo wa toba). Hebu tufungue I Wakorintho. . . nakusudia, hebu tufungue Matendo, sura ya 19, kwa muda mchache. Na tusome haya kwa dakika moja hivi ili muone, marafiki,

hilo si-si . . . sisi si . . . Maandiko hayahitilafiani yenyewe. Vema, tazama hapa:

Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, . . . akiisha kupita kati ya nchi za juu . . . Efeso, akakutana na wanafunzi kadha wa kadha huko;

Akawauliza; Je! mlipokea Roho Mtakatifu tangu mliipoamini? . . . wakamjibu . . . hata kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia.

. . . akawauliza, . . . basi mlibatizwa kwa ubatizo gani?

Ee, walisema, tumebatizwa.

Kasema, vipi?

. . . wakasema, kwa Yohana, Yohana . . .

Yeye alisema, Yohana alibatiza tu ubatizo wa toba, akiwaambia akisema *ya kwamba* inawapasa kumwamini yeye aliyekuja . . . *atakayekuja yaani*, Bwana Yesu Kristo.

Waliposikia haya wakabatizwa tena kwa jina la Yesu Kristo.

. . . Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri.

223 Kisha Mtakatifu mashuhuri Paulo . . .

224 Sikiza! Vipi kama ulikuwa umebatizwa na Yohana Mbatizaji, mtu yule yule aliyembatiza Yesu Kristo? Mtu mtakatifu, ambapo Yesu alisema, “Hakujawahi kuwa na mtu aliyezaliwa na mwanamke aliye mkuu kama Yohana Mbatizaji.” Yeye ni mkuu wa manabii wote. Alimpeleka Yesu majini na akambatiza mumo humo Yordani. Ndugu, kama nilibatizwa naye, ningejisikia vizuri sana. Sivyo?

225 Lakini Paulo ageuka na kusema, “Huo haufai sasa!” Kasema, “Yawapasa mbatizwe tena.”

226 “Ee, tumezikwa katika maji mengi, ingawaje, Paulo! Tulibatizwa kwa maji mengi na Yohana, kule katika Mto Yordani.”

227 Yeye alisema, “Huo hautendi kazi sasa. Yawapasa mbatizwe tena.”

“Vipi?”

228 Kasema, “Yohana alibatiza ubatizo wa toba. Huu ni kwa ondoleo la dhambi, na hakuna jina lingine chini ya Mbingu alilowapa mwanadamu, isipokuwa Jina la Yesu Kristo.” Nao iliwapasa wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo.

229 Hakuna hata mahali pamoja katika Biblia, au historia yote kwa miaka mia sita baada ya kifo cha mtume wa mwisho,

waliwahi kubatiza kwa njia iwayo yote ila kwa Jina la Yesu Kristo.

²³⁰ Na enda kamuulize kasisi Mkatoliki ye yote utakaye, waulize nani aliyegeuza hayo, na uone watakayokwambia. Chukua katekisimu na ukaisome; kasema, “Hakika, baadhi ya Waprotestanti wataokoka kwa sababu wanakubaliana na ubatizo wetu.” Waliubadili. Wanasema wana nguvu na mamlaka kufanya hilo, nanyi mwaliadini! Hivyo ndivyo wasemavyo, hivyo ndivyo wanavyodai, kanisa Protestanti hukubali. Lakini, Kimaandiko, hakuna kabisa hata wakia moja ya Maandiko kuhusu hilo.

Iliwapasa wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo!

²³¹ Sasa sikiza, upesi sasa, ili tulipate vyema...Sitaki kuwakawisha sana kwa maswali haya. Tazama, katika siku ambayo Yesu alishuka kutoka Mlima wa Kugeuzwa pamoja na wanafunzi Wake, Yeye alisema, “Watu husema Mimi ni nani, nao husemaje?”

²³² “Wengine hunena kuwa, ‘Wewe u Yohana Mbatizaji,’ wengine hunena wewe u ‘Eliya,’ na wengine hunena wewe ‘u nabii yule.’”

Yeye alisema, “Lakini nanyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?”

²³³ Na Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

²³⁴ Yeye akasema, “Heri wewe Simoni—Simoni Bar-yona,” kasema, “kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza kwa kanisa fulani, hukujifunza haya kwa seminari fulani. Kwa sababu Baba Yangu amekufunulia wewe hili, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu na malango ya kusimu hayatalishinda.”

²³⁵ Sasa, kanisa Katoliki husema, “Ilikuwa ni Petro. Walikuwa na mwamba pale, na bado uko pale chini ya Mji wa Vatikani,” (na hiyo ilikuwa katika Yerusalemu, katika Upalestina). Nao walisema huo ndio mwamba.

²³⁶ Kanisa Protestanti husema, “Walijenga Kanisa juu ya Petro.” Kama ndivyo ilivyo, basi lilianguka siku chache baadaye. Haikuwa hivyo.

²³⁷ Kanisa limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu wa Mungu. Mwili na damu havikukufunulia wewe, Petro, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia wewe. Na juu ya mwamba huu (ufunuo wa kiroho wa Neno la Mungu) nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda.

²³⁸ Hapo ndipo nasema, katika Luther, Methodisti, na vyo vyote ulivyo, vyo vyote vile, Wapentekoste, na vyo vyote ulivyo, haijalishi kamwe; Kanisa la Mungu linapoendelea katika nguvu za kutiwa pumzi, litaendelea na kuendela na kuendelea moja

kwa moja. Na hakuna dhehebu linaloweza kulikomesha, hakuna cho chote ulimwenguni kitakachoweza kulikomesha. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.” Ukweli wa Kiroho, uliofunuliwa!

²³⁹ Sasa chunguza kifungu kifuatacho, Yeye asema, “Na wewe ndiwe Simoni, na nitakupa wewe...” kwa sababu alikuwa na Ukweli wa kiroho, uliofunuliwa. Hiyo ndiyo sababu alijua tofauti kati ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na Jina la Bwana Yesu Kristo. Yeye alikuwa na ufunuo wa kiroho. Hivyo ndivyo unavyoelewa, usiku huu, ambapo Roho Mtakatifu anatufunulia sisi.

²⁴⁰ Yeye alisema, “Wewe ndiwe Simoni, nami nitakupa wewe funguo za Ufalme wa Mbinguni. Na lo lote utakalolifunga duniani hapa, nitalifunga Mbinguni. Lo lote ufungualo duniani humu, nitaifungua Mbinguni.” Je, Yeye alisema haya? Mathayo Mt., sura ya 16, “Lo lote utakalolifungua duniani, nitalifunga Mbinguni. Lo lote utakalolifungua duniani, nitalifunga Mbinguni. Nami nitakupa funguo za” (nini?) “Ufalme wa Mbinguni.” Ufalme wa Mbinguni ni nini? Roho Mtakatifu! Biblia ilisema, “Ufalme wa Mbinguni u ndani yenu...” Namaanisha “Ufalme wa Mungu.” Samahani. “Ufalme u ndani yenu.”

²⁴¹ Sasa, Yeye alisema, “Wengine wasimamao hapa hawataonja mauti hata watakapouona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu.” Siku chache tu baadaye ilikuwa Pentekoste, Ona? “Wengine wasimamao hapa,” mahali papo hapo, akisema aliyokuwa akisema. “Wengine wenu mnaosimama hapa...” Yeye alikuwa tu amegezwa, kasema, “Hamtaonja mauti hata mtakapouona Ufalme wa Mungu ukija katika nguvu.”

²⁴² Biblia ilisema “Ufalme u ndani yenu.” Yesu alipofufuka toka kwa wafu, kumbuka, Yeye alikuwa na funguo za mauti na kuzimu, si funguo za Ufalme, hizo zilikwisha kupewa Kanisa. Sasa, Petro alikuwa na funguo zile. Je, mwaamini Yesu angetimiza Neno Lake? Asipolitimiza, ndugu, Yeye hakuwa Mungu! Hivyo tu. Sasa, Yeye alisema, “Petro, nitakupa funguo za Ufalme,” yaani, “za Roho Mtakatifu. Lo lote utakalofunga duniani, nitalifunga Mbinguni.”

²⁴³ Sasa tazama kosa walilofanya, kutoka nje na kusamehe dhambi na mengineyo kama hayo. Ni kosa jinsi gani! Hebu tuone. Walimpa yeye hizo funguo. Sasa, Yeye alielekeza uso wake moja kwa moja kwa Pente... au moja kwa moja kuelekea Yerusalemu.

²⁴⁴ Yeye akasulubiwa, akafa, akafufuka siku ya tatu, alikuwa duniani siku arobaini miongoni mwa watu, akapaa Mbinguni. Akawaambia wangoje hata Ufalme wa Mungu ukija kati yao, wakati huu Baba atarudisha Ufalme katika hali ya kiroho kwao. Wao wakaenda katika nji wa Yerusalemu na kungoja kule kwa siku arobaini mchana na usiku, na, kwa ghafula, ubatizo wa

Roho Mtakatifu (Ufalme wa Mungu) ukuja kwa nguvu juu yao. Sivyoy?

²⁴⁵ Sasa tazama! Petro, asiyeelimika, hata hangaliandika jina lake (papa? naam, papa), alisimama juu ya kijisanduku kidogo cha sabuni au kitu fulani na kuanza kuhubiri. Yeye alisema, “Enyi watu wa Uyahudi na ninyi nyote mkao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize Maneno yangu. Sivyoy mnavyodhani; watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli, ‘Itakuwa siku za mwisho,’ asema Mungu, ‘nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri; na watumishi Wangu wanaume kwa wanawake nitawamwagia Roho Yangu, nao watatabiri. Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini, moto, nguzo ya moto, na mvuke wa moshi.’” Akaendelea, akinena kuhusu Daudi na wengineo.

²⁴⁶ Na hawa wakinzani waliposimama pale, ndipo wakasema, “Waume na ndugu zetu, tutendeje tupate kuokoka?”

²⁴⁷ “Lo jihadhari Petro, una funguo zinazonig’inia pale sasa.” Sivyoy? Ujumbe wa kwanza wa Injili!

²⁴⁸ Yesu, siku chache hapo kabla, kabla hajasulubishwa, alisema, “Petro, nitakupa funguo. Lo lote utakalofunga, nitalifunga; lo lote utakalofungua, nitalifungua. Au lo lote utakalotenda, nitalitambua Mbinguni.” Kama Yeye ni Mtu wa Neno Lake, Yeye atatimiza Neno Lake!

²⁴⁹ Ndiye huyu amesimama hapa, Roho Mtakatifu alikuwa ameshuka kwa mara Yake ya kwanza, na Petro aliulizwa, “Tutendeje tupate kuokoka?”

²⁵⁰ “Tahadhari, unaingiza ufunguo katika Ufalme kwa mara ya kwanza. Yesu alikwambieni, siku chache zilizopita, ilikuwa siku kumi zilizopita, kasema, ‘Endeni mkabatize watu kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’ Utafanyaje? Lakini alikupa wewe funguo hizo kwa sababu ulikuwa na ufunuo wa kiroho! Kwa maana Kanisa Langu litajengwa, na milango ya kuzimu haitalishinda.”

²⁵¹ Na chukua kanuni zako za imani na mafundisho yako, na cho chote utakacho, lakini vitashindwa vibaya sana (imekuwa hivyo), lakini nguvu za Mungu Aishiye zitaendelea na kuendelea hata kitaka Umilele. Kama mwali wa madini ya radium, linaendelea (tazama) bila kikomo.

²⁵² “Petro, una funguo. Lo lote utendalo hapa, hapana shaka Mungu atalitambua Mbinguni.” Sivyoy? “Unasemaje, Petro? Tutendeje tupate kuokoka?”

²⁵³ Petro alisema. . . Msiende mkasema, “*Mariam Mtakatifu*,” hakuna jambo kama hilo, kufanya sala za siku tisa. Usije na kusalimiana kwa mikono na kuandika jina lako katika kitabu cha kanisa na uwakubalie wakunyunyuzie maji kidogo, hakuna

cha hiyo. Hayo ni mafundisho ya sharti ya Katoliki ambayo kanisa Protestanti linakubaliana na nayo.

254 Yeye hakusema, “Ninyi nyote nendeni... Na sasa, Yesu aliniambia siku chache zilizopita, kuwa nyote muende mkabatizwe kwa jina la ‘Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.’ Si mtu aliye na ufunuo wa kiroho, hangalisema hayo.

255 Yeye alisema, “Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Naam. Kisha ufunguo ukaingia ndani na kufunga, ukafungwa Mbinguni!

256 Hiyo ndiyo sababu Paulo aliwaambia wanafunzi wa Yohana, “Yawapasa mbatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo, ili mpokee ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

257 Hukujua hilo hapo kabla, unalijua sasa! Jamani! Ni vema. Hiyo ni juu yako. Hilo ni kweli. Lakini wa kiutatu, ubatizo wa utatu haukutambuliwa kamwe Kanisani, Agano Jipya; ila tu katika kanisa Katoliki, na kanisa Protestanti linakubaliana na hayo. Tazama! watu wengi wangekugombanisha kwa hayo. Lakini ndugu, yakupasa ujikatie kauli wewe mwenyewe.

258 Sasa unasema, “Ndugu Branham, nilibatizwa kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Nimepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.”

259 Sishuku neno lako. Sina sababu yo yote ya kushuku neno lako, naliadini. Naamini Mungu aliwapa hao Roho Mtakatifu juu pale kabla wao hawajabatizwa kwa vyo vyote vile; lakini Petro alipowaambia la kufanya, walienda na kulitenda. Hiyo ni kweli. Sasa mnajua la kutenda, naam; na kama ukikataa kutembea katika Nuru Nuru inapoletwa, unaingia gizani. Vema! Amina! Naam. Kuniradhi. Sitaki mniradhi kwa kupiga shangwe “na iwe hivyo” kwa Neno la Mungu. La, bwana. Nitapiga shangwe tena “Amina.” Naam, bwana.

Mbona wabatiza kwa Jina la Yesu Kristo, Ndugu Branham? Mbona unatenda hilo badala ya “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu”? Kwa sababu Biblia hufundisha hivyo! Je, hilo ni dhahiri?

Mbona mnatawadhana miguu, Ndugu Branham? Kwa maana, Biblia hufundisha hilo, naamini Injili nzima.

Vema sasa: **Ubatizo wa uongo ulionena juu yake ni upi?** Naam. Ndio huo hasa. Hauko po pote... Soma tena katika Agano na upate ambapo mtu mmoja...

260 Sasa kwenu watu wapendwa, siumizi dhamiri zenu, sitaki kufanya hivyo. Nawauliza muwe wanyenyekevu na si... Tazama kitu hiki waziwazi, na uone kinaonekanaje. Kitazame kulingana

na Biblia, si kulingana na kanisa lako wala upumbavu fulani, kitu fulani cha ujinga mtu fulani amekijaza kichwani mwake, lakini tazama Neno la Mungu. Hakika!

²⁶¹ Je, wadhani Mungu Mwenyezi angenipa huduma Yeye aliyo nayo humu namna hii, pamoja na ishara za kimbunguni na mengineyo ambayo hayajawahi kuonekana tangu Agano Jipya, na aniache nienende kwa kosa hivyo? Haiwezekani kamwe! Na, ndugu, nitakapotoka ng'ambo nitaweka sehemu kubwa ya wakati wangu si kwa uponyaji wa Kiungu na miujiza bali kuhubiri Neno la Mungu. Naam hasa.

Basi, tuone!

38. Je, kanisa lafundisha kuwa yakupasa unene kwa lugha kumpokea Roho Mtakatifu?

²⁶² La, bwana. La, hatufundishi hivyo. Kunena kwa lugha ni karama ya Roho Mtakatifu, ona, si Roho Mtakatifu. Ni karama. mti huu huzaa matunda namna tisa. Sivyo?

²⁶³ Kama ukiangalia mtofaa, una matofaa, utasema ni mtofaa. Utazame mti, una mapera, utasema ni mpera. Haijalishi kama una maganda ya mkuyu, ukiwa una mapera, uhai wake ni upi? Uhai wake ni wa mpera. Sivyo?

²⁶⁴ Sasa, huu Mti wa Mungu huzaa aina tisa za matunda ya kiroho. Sivyo? Vema. Zote ni tofauti. . . kasema, “Mmoja alipewa mafundi. . . maarifa, hekima, ufahamu, na kunena kwa lugha, tafsiri ya lugha,” karama tisa za kiroho mbalimbali huota kwenye Mti huu wa Mungu. Sivyo? Vema, sasa, kunena tu kwa lugha silo la pekee, kuna mengine humo pia.

²⁶⁵ Sasa, unaweza kunena kwa lugha na bado usiwe na Roho Mtakatifu. Sasa, kumbuka tu hilo. Nimekuwa hapo. . . nimewaona walozi na wachawi wakija na kunena kwa lugha, nao hawana Roho Mtakatifu. Wajua, nimewaona wao wakija wakipiga vigelegele na kuruka, nao hawana Roho Mtakatifu. Nilisimama katika ngoma za mahindi hapa si muda mrefu uliopita, nje mbali kidogo na Douglas, Arizona, nje kule. Niliona hizo ngoma za mahindi wanapokuwa nazo juu pale, na mchawi huyo akaja pale na akatenda mambo ya kutisha, na kila kitu, akaendelea na—akatupa uchafu ndani mle. Hilo halikumaaanisha yeye alikuwa ameokolewa. Mtu huyo alikuwa m—mchawi.

²⁶⁶ Nilisimama India. . . Afrika na kuona wachawi wakija na kubishana nami hivyo, na uchawi wao, na hata kunywea damu kwenye fuvu la kichwa. Naam. Inakupasa kujua vema zaidi yale unayoongea unapokabiliana na hayo. Lakini nimeona nguvu za Mwenyezi Mungu zikimfunga mtu huyo hata asiweze kusonga mbele; kwa hivyo basi anakukodolea macho hivyo, na wakambeba kumwondoa. Naam, bwana.

²⁶⁷ Ndugu, Mungu ni wa kweli! Naam. Lakini Mungu ni Roho, hakomei tu kwa kunena kwa lugha au *hiki, kile wala kinginecho*.

Nasema mtu ye yote aliye. . . Hiyo ndiyo shida kanisani hapa. Ona, Pentekoste ilikosea kwa hilo jambo moja.

Walifikia mahali ambapo watu. . . Badala ya—ya kuwawekea mikono, nao kumpokea Roho Mtakatifu, waliwaleta madhabahuni na kuanza kuwapigapiga mgongoni na kusema, “Iseme, Iseme, Iseme!” na kurudia-rudia neno tena na tena, hata wakapata farakano na si lugha.

²⁶⁸ Kama mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu halisi amezaliwa na Roho wa Mungu, yeye ataishi maisha ya kiungu. Baadhi ya watu, waliishi maisha ya kutisha, nanyi mwajua hilo, na matunda yao yalithibitisha hawakuwa hivyo. Yesu alisema, “Kwa matunda yao mtawajua.” Na tunda la Roho si kunena kwa lugha, hiyo ni karama ya Roho.

²⁶⁹ Petro hakusema kamwe, “Tubuni, mkabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo, nanyi mtapokea Roho Mtakatifu,” yeye alisema, “Nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu,” waliposikia lugha hizi na watu wakinena. Ni mojawapo wa karama za Roho Mtakatifu walizopokea. Amina. Vema, Yanipasa niharakishie.

39. Nina wana wa kiume wawili (mmoja, umri wa maika miwili; na mwingine, mitano), nao wamenyunyuziwa. Je, yawapasa hao wabatizwe kwa kuzikwa majini?

²⁷⁰ Vema, sasa, dada au ndugu, ye yote uliye, hayo ni juu yako. Nina binti mdogo. . . Mwanangu mdogo, Billy Paul, alikuwa na umri wa maika kumi na sita, nami nilimbatiza kwa Jina la Bwana Yesu papa hapa. Binti yangu alikuwa na umri wa miaka minane; yeye alinijia—na akakaa pajani mwangu, naye akasema, “Baba, nataka kumwamini Bwana Yesu Kristo, nami—nataka, kubatizwa.” Nami nilimbatiza huyo msichana mdogo wa umri wa miaka minane. Na kama hawa watoto wadogo wataka kubatizwa, wabatizeni. Kama hawataki, naam, kama wana. . . endelea mbele, hilo ni juu yako, lo lote Bwana alilosema.

40. Je, ni wale pekee walio na ubatizo wa Roho Mtakatifu watakaokuwa katika Kunyakuliwa kwa Kanisa, au waamini wote watadhihirishwa?

²⁷¹ Hatu. . . hatuna wakati wa kuthibitisha hilo. Lakini, ndugu, ni Bibi-arusi wa Roho Mtakatifu pekee atakayekuwa katika Kunyakuliwa ona? Biblia. . . ?. . . wengine hawatapotea.

²⁷² Tazama! Nani atakayehukumu dunia? Watakatifu. Danieli alisema, “Na nikaona Yeye akija kwa yule Mzee wa Siku, na—naye akaja na kumi elfu mara kumi elfu ya watakatifu Wake.” Sivyo? Kunyakuliwa, Kanisa lilikuwa limeondoka. Ndipo wakashuka chini, na Hukumu ikawekwa.

²⁷³ Na Vitabu vikafunguliwa. Sivyo? Na Kitabu kingine kikafunguliwa ambacho ni Kitabu cha Uzima (waamini

waliotakaswa ambao hawakuwa wamempokea Roho Mtakatifu).

²⁷⁴ Si Yesu alifundisha kuwa wanawali kumi walienda kumlaki Bwana arusi, na watano wao...? Au hao wote walikuwa wanawali, wasafi na watakatifu. Nao... *Hawa* walienda kulala na hawakumpokea Roho Mtakatifu: na *hawa* wakampokea Roho Mtakatifu na walikuwa na Mafuta taani mwao. Na Bwana arusi alipokuja, Sauti ikaja, ikipaswa, wao wakasema, “Hima, twendeni. Na tupeni Mafuta yenu kidogo!”

²⁷⁵ Yeye alisema, “Shikeni njia mwende mkanunue, ombeni sana, mmpokee sasa.” Lakini hawakuweza. Nao walipokuwa wakienda, wale—wale wanawali waliingia katika Karamu ya Arusi nao hao walitupwa katika giza ambako walikuwa wakilia na kuomboleza na kusaga memo. Si Ufunuo, usiku uliopita katika sura ya 12, usiku wa juzi, ilifundisha kuwa yule joka kubwa jekundu alitoa katika kinywa chake maji kufanya vita na Wazao wa mwanamke *waliosalia*, waliokuwa na imani kwa Mungu na wazishikao amri za Yesu Kristo?

²⁷⁶ Kweni wanawake, mnapotandaa mshono wenu. Ni kitambaa kizuri cha jora, jora ile ile ndani yake, lakini wewe waichukua *hii* na kuweka mshono wako jinsi tu utakavyokikata. Ndiposa unakikata. Hayo ni juu yako. Lakini unachukua kitambaa ulichokata, kutengenezea vazi lako, na kinachobakia kinatumiwa. Ni kitambaa kizuri tu kama kitambaa kingine cho chote, lakini kwa uchaguzi umechagua *hicho*. Sivyo? Kingine kilichobaki ni kitakatifu na kizuri tu kama hicho, na cha thamani tu kama kile kilichobakia, lakini hilo lilikuwa chaguo lako.

²⁷⁷ Na Mungu ameahidi kuwa tutanyakuliwa kwa uchaguzi! Na Biblia ilisema, “Na hao wafu waliosalia hawakuwa hai kwa miaka elfu moja.” Sivyo? Kwa hivyo... Hutapotea, bali Bibi-arusi aliyejazwa Roho Mtakatifu ataenda katika Kunyakuliwa. Wengine wao watapitia Hukumuni; hali Wao hawakupitia.

41. Kama unapaswa kubatizwa kwa Jina la Yesu, mbona Yesu aseme katika Mathayo 28, mbatizwe kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu?” Hilo ndilo nimetoka kueleza sasa hivi, hilo.

²⁷⁸ Vema, mnachoka? Najua mnachoka. Lakini:

42. Je, Mungu haheshimu ubatizo wa “Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu?” Si kuna watu wanobatizwa kwa jina, kwa majina haya ambao wamempokea Roho Mtakatifu? Je, Yesu alikuja kumtukuza Baba? Si ubatizo huu ungetambuliwa?

²⁷⁹ Naam, Yesu alikuja kumtukuza Baba, tazama katika Yohana Mt. sura ya 14. Mimi ni karibu... Nina... kama mtangoja tu matatu zaidi, tutamaliza, naamini. Tazama, na ndipo tuna mengine mapya kesho. Amina. Kwa sababu nitapata mengine

kutokana na usiku huu, naamini. Tazama, mimi . . . kanisa hili lina, ingawaje, hili lingali linaendelea.

280 Tazama, Yesu alikuja kumdhihirisha Baba. Tazama, hapo mwanzo, Mungu alimuumba mtu kwa mfano Wake. Sivyo? Vema, Mungu ni nani? Roho. Yohana Mt. sura ya 4, Yesu akisema na yule mama kule kisimani, Yeye alisema, “Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yawapasa wamwabudu katika Roho na Kweli.” Sivyo? Kama Mungu alimuumba mtu kwa mfano Wake, Yeye alimuumba mtu aina gani? Mtu roho.

281 Katika Mwanzo 2, hakukuwa na mtu wa kulima ardhi, na Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi; si kwa mfano Wake, lakini mfano wa uhai wa wanyama. Naye akaiweka roho ya mwanadamu katika huyu mtu mnyama hapa, naye akawa nafsi hai. Sasa hiyo ndiyo tofauti kati ya mwanadamu na mnyama. Mnyama haundi motokaa, naye hafanyi mambo kama hayo kupata riziki yake na mengineyo kama hayo. Yeye ni mnyama, mnyama bubu, yeye hana nafsi. Yeye hawezi kusoma na kuandika, hawezi kunena, kuongea, yeye ni mnyama bubu. Lakini mwanadamu ana mwili kama wa mnyama bali yeye ana nafsi ya Mungu ndani yake imfanyayo asiye kufa. Naye aweza kuvumbua, tazama yale yeye awezaye kutenda! Yeye ana . . . karibu hali sawa na Mungu, kwa sababu yu mwana wa Mungu hata katika hali yake ya kuanguka. Yeye ni wa ajabu! Mtazame! Ona? Naam.

282 Ndipo mwanadamu alipoanguka katika mwili . . . Na kama Mungu angemtuma mtu mwingine mbali naye Mwenyewe, Yeye hakuwa wa haki. Njia pekee Mungu angelifanya ni kupachukua mahali pa mwanadamu binafsi.

283 Vipi kama nilimfanya Ndugu Neville afe kwa ajili ya mwanamke huyu hapa? Vipi kama nilimfanya mwanamke huyu afe kwa ajili ya mwanamke huyu hapa, kama ningalikuwa nawatawala? Singekuwa mwenye haki na nifanye hilo. Kama ningalitangaza kifo, na nataka uishi, yanipasa nichukue mahali pako kukuhesabia wewe haki.

284 Ndiposa Mungu aliyekuwa katika mfano wa Roho, bila umbo, samahani, Biblia ilisema, “Mungu asiye na umbo.” Vema. Ndipo Mungu ilimbidi achukue umbo, na Yeye alimfunika kama uvuli bikira na kuumba ndani yake chembechembe hai ya damu, bila kujuana kimwili wala lo lote lile, na kuumba chembechembe hai ya damu iliyokua ikawa Mwana wa Mungu. Kisha Mungu akashuka na kukaa katika Mwanawe, Kristo Yesu, akimfanya Yeye Mungu duniani.

285 Wakati Yohana Mt. . . . Tomaso alisema, “Bwana, tuonyeshe Baba, yatutosha.”

286 Yeye alisema, “Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku zote, wewe usinijue?” Yeye akasema, “Basi wewe wasemaje, ‘Utuonyeshe Baba?’” Naam, Yeye alisema, “Ukionia Mimi

umemwona Baba. Mimi na Baba tu Mmoja. Baba Yangu yu ndani Yangu.”

287 Bibi fulani, hapa si muda mrefu umepita, nilikuwa nikinena pale, akaruka juu, kasema, “Ee Ndugu Branham,” kasema, “Ninajua yale unayomaanisha. Hao ni mmoja, hakika hao ni mmoja.” Kasema, “Wewe na mke wako ni mmoja, pia. Huo ndio umoja walio nao.”

288 Nikasema, “Samahani,” Nikasema, “hawako hivyo.” Nikamwuliza, “Je, unaniona mimi?”

Kasema, “Hakika.”

Nikasema, “Je, unamwona mke wangu?”

Kasema, “La.”

289 Nami nilisema “Pale! Basi wao ni umoja tofauti na umoja wangu na mke wangu.” Ona? Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

290 Yesu alisema, “Huwezi kuniona Mimi pasipo kumwona Baba.” Hakika huwezi! Ni sehemu ya pili ya kile kijiti cha kupimia cha futi tatu, kijiti kile kile. Ni Mungu. Yesu Kristo alikuwa Mungu, la sivyo, mdanganyajifu mkuu sana ulimwenguni uliyewahi kupata.

291 Sikiza! Mwanamke fulani aliniambia si muda mwingi umepita, “Nitakuthibitishia,” mwanamke wa Christian Science. Naam, marafiki mlilo wa Christian Science, tulieni tu kwa dakika moja hivi, ona. Wao walisema, “Nitakuthibitishia wewe kuwa Yeye hakuwa cho chote ila mwanadamu.” Kasema, “Unamwinua sana Yesu.”

292 Nilimwambia “Hata nikisifu mchana na usiku singeweza kumpa zile Yeye anazostahili.” Nilisema, “Si ajabu. . .”

293 Naam, Isaya alijaribu kumpa Jina, yeye alisema, “Yeye ni Mshauri, wa Ajabu, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa milele.” Hayo yote! “Yeye ni Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho, Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi Inayong’aa. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.” “Katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili,” Biblia ilisema. Utimilifu wa Mungu ulikuwa katika Yeye!

294 Yeye alisema, “Nitakwambia, Yeye alipoenda kumwomba Lazoro, kumfufua Lazoro,” kasema, “nitakuthibitishia kuwa Yeye alikuwa mwanadamu tu.”

295 Nikasema, “Hebu nione ukifanya hayo”!

296 Kasema, “Biblia ilisema, ‘Alilia.’ Na hilo lathibitisha kuwa yeye alikuwa mwanadamu, Yeye angelia.”

297 Nikasemasema, “Hakika, huyo aliyekuwa akilia alikuwa Mwana.”

298 Yeye alikuwa Mungu-Mwanadamu. Yeye alikuwa kiumbe cha kiutatu kama nilivyo mimi, ulivyo; sisi tu nafsi, mwili, na roho. Yeye alikuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu,

katika Ungu wa Mungu; hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa. Yeye alikuwa Ungu Mwenyewe! Yeye angeweza kufanya lo lote pale wakati ile... Watoto Wake mwenyewe wakililia damu Yake? Kama ingekuwa mtu mwingine... Hao walikuwa watoto Waje Mwenyewe wakililia damu Yake, si ajabu Yeye aliwalilia. Mtu angeweza... na watoto Wake wakililia damu Yake, Yeye angejisikiaje? Au awahukumu waende kuzimuni milele, au atoe Uhai Wake; Yeye alikuwa Mungu akitoa uhai Wake kwa ajili ya watoto wake! Ungu ulikaa ndani Yake! Hivyo ndivyo Yeye alivyokuwa.

²⁹⁹ Mwanamke huyo akasema, “Tazama,” kasema, “Mchungaji Branham, nitakuthibitisha wewe! Yeye alipolia, ilithibitisha alikuwa mwanadamu.”

³⁰⁰ Nikasema, “Bibi, Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa aki... alipokuwa akilia, naam. Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa akilia, lakini alipounyosha mwili Wake mdhaifu na kumwambia mtu aliyekuwa amekufa kwa siku nne, “Lazaro amka!” Na mtu yule aliyekuwa amekufa kwa siku nne, na ameoza, na wadudu wa mwilini wakitambaa-tambaa ndani yake, uharibifu ulimjua Bwana Wake na nafsi ilimjua Muumba Wake, na sasa mtu aliyekuwa amekufa kwa siku nne alisimama kwa miguu yake na kuishi tena! Huyu alikuwa zaidi ya mwanadamu!”

³⁰¹ Yeye alikuwa mwanadamu wakati aliposhuka toka mlimani usiku huo, akiwa na njaa, akitazama juu ya mti fulani apate kitu cha kula. Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa akitafuta mle kitu cho chote ale kwenye ule mtini. Lakini alipochukua biskuti tano na vipande viwili vya samaki na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu! Huyu alikuwa Mungu katika mwanadamu! Yule Muumba ambaye angechukua samaki iliyopikwa na kuivunja-vunja na ilikuwa bado samaki iliyopikwa, akautwaa mkate uliookwa na kuuvunja-vunja, je, Yeye aliachilia atomi aina gani? Haleluya! Yeye alikuwa Mungu, Muumba wa atomi na vitu vyote! Huyu alikuwa zaidi ya mwanadamu!

³⁰² Yeye alikuwa mwanadamu alipokuwa nje kule katika mtumbwi usiku huo baada ya kuhubiri siku nzima na kuwaponya wagonjwa, mchovu sana, hata pepo elfu kumi wa baharini waliapa wangemzamisha. Maskini mtumbwi huo mdogo na mkuukuu nje pale ukirushwa-rushwa hapa na pale kama kizibo cha chupa, mawimbi makubwa yakipiga hapa na pale, na Yeye amelala, amechoka sana hata mawimbi hayo hayakumuamsha. Shetani alikuwa akinguruma, kasema, “Tutampata sasa ali analala.” Lakini Yeye alipoamka, akaamka pale, alikuwa mwanadamu, alikuwa mchovu sana. Lakini alipoweka mguu Wake kwenye kizingiti cha mtumbwi, Yeye akaiambia bahari hiyo, “Tulia!” na upepo na mawimbi vikamtii.

Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu! Huyo alikuwa Mungu, Muumba aliyumba Mbingu.

303 Si ajabu mitume walisema, “Ni nani huyu, basi, hata upepo na mawimbi vinamtii!”

304 Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa Mungu. Yeye alikuwa mwanadamu alipotundikwa msalabani kama Toleo kuondoa dhambi. Yeye alikuwa mwanadamu huku amepigiliwa misumari mikononi Mwake. Yeye alikuwa mwanadamu mwenye miiba kichwani Mwake. Yeye alikuwa mwanadamu ambaye askari wenye dhihaka walimtemea mate. Yeye alikuwa mwanadamu aliyechubuliwa, akavuliwa nguo na kujeruhiwa. Yeye alikuwa mwanadamu! Yeye alikuwa mwanadamu alipolia, “Mungu Wangu, mbona umeniacha?” Yeye alikuwa mwanadamu akiomba msaada. Lakini katika asubuhi ya Pasaka wakati zile mihuri za mauti zilipofunguka mle Kaburini, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu! Yeye alithibitisha ya kuwa alikuwa Mungu.

Maishani, alinipenda, kufani, akaniokoa
Alipozikwa, akaondolea mbali dhambi zangu;
Alipofufuka, akanihesabia haki bure milele.
Yujaja siku moja, Ee, siku tukufu.

Lo, huku miamba ikipasuka na mbingu
zikitiwa giza,
Mwokozi wangu aliinamisha kichwa chake
akafa;
Pazia lililofunguka lilionyesha njia
Ya kuingia kwenye raha za Mbinguni na siku
isiyo na mwisho.

305 Si ajabu Eddie Pruitt alipaza sauti:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!
Na malaika wamsujudie,
Ileteni taji ya kifalme
Mkamvike taji Bwana wa wote.

306 Huyo ndiye yule Mtu mkuu, Bwana Yesu. Yeye alikuwa Yehova, Mungu aliyejificha katika mwili. Biblia ilisema, “Kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote kwa Jina lake.” Biblia ilisema, “Jamaa yote Mbinguni inaitwa ‘Yesu,’ na jamaa yote duniani inaitwa ‘Yesu.’” Hebu tuombe kwa Jina Lake, tuishi kwa Jina Lake, tubatizwe kwa Jina Lake, tufufuke kwa Jina Lake, tuende Mbinguni kwa Jina Lake. Hilo ni Jina Lake, na Bibi-arusi Wake anaitwa “Bi. Yesu.” Yeye atatwaa watu toka kwa Mataifa kwa ajili ya Jina Lake.

307 Nami si wa umoja. La, bwana. Ninyi wa utatu tupilieni hilo mbali. Mimi si wa umoja. La, bwana. Mimi si wa umoja wala wa utatu. Naamini Biblia isemavyo. Hiyo ni kweli. Amina. Jamani! Nimechukua muda mwingi sana kwa moja. Hilo lilikuwa nini? Je, nimelieleza? Au, hebu tuone, ilikuwa nini? Lo, naam, hiyo ni

kweli, kuhusu. . . jinsi Baba alivyokuwa ndani ya Kristo. Yeye alikuwa mwanadamu, Yeye alikuwa Mungu-mwanadamu.

43. Si kanisa Pentekoste hubatiza kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu? Baadhi yayo.

44. Mtu akifa pasipo ubatizo wa Roho Mtakatifu, je, atapotea?

³⁰⁸ La, bwana. Kama yeye ni mwamini yeye atakuja katika ufufuo, ule ufufuo wa pili. Kama yeye ana huo ubatizo, yeye ataenda katika ufufuo wa kwanza. Sasa, itakulazimu kusadiki neno langu. Kama hilo halitoshelezi, basi uni—uniulize, nitakupa Andiko lake. Ninajaribu kupata haya mawili au matatu zaidi hapa, ndipo tutamaliza.

45. Ndugu Bill, Biblia husema lo lote kuhusu kucheza kamari?

³⁰⁹ Naam, inasema, lakini siwezi kukumbuka hivi sasa. Najua askari walichezea mavazi Yake, kamari, na mengineyo kama hayo, lakini siwezi kupataja.

46. Tafadhali fafuanua I Wakorintho 15:29?

³¹⁰ Nifungulie pale, ukiweza, Ndugu Neville, I Wakorintho 15:29. Tutapata hilo.

³¹¹ Sasa, labda kesho naweza kuwaletae ninyi hilo tena. Kama hizo—hizo herufi mnazoendeleza, “VICARIVS FILLI DEI.” mkitaka, nijulisheni.

47. Je, unabii wa Ezekieli 38 na 39 utatimia kabla ya Kunyakuliwa?

³¹² Nadhani sivyo. Nadhani kitu kinachofuata tunachotazamia ni Kunyakuliwa kwa Kanisa. Ndiposa “wakati Gogu na Magogu watakapokuja” ni majeshi ya Urusi yanayokuja baada ya . . .

³¹³ Tazama! Bw. Bohanon, aliyekuwa msimamizi hapa katika Shirika la Umma, Mkristo mwema sana. Naye aliongea nami siku moja, akasema, “Billy, nilijaribu kusoma, nami nilijaribu kumwuliza mchungaji wangu afafanue Ufunuo.” Kasema, “Tukafikia pale nasi tukatatanishwa.” Kasema, “Yohana bila shaka alikuwa akila kitu—kitu fulani usiku huo na akawa na ndoto.”

³¹⁴ Nilisema, “Bw. Bohanon, huna haya.” Nilisema . . .

Yeye akasema, “Vema, hakuna ye yote anayeweza kufahamu Huo.”

Nilisema, “Hakuna mwanadamu wa kawaida, ila Roho Mtakatifu aweza kuufunua.”

³¹⁵ Yeye akasema, “Vema, tazama hapa, Billy.” Yeye kasema, “Bibi-arusi alikuwa amesimama kwenye Mlima Sinai. Na hapa kulikuwa na maji yaliyotoka kinywani mwa lile joka kubwa kufanya na kuleta vita kwa Bibi-arusi. Naye Bibi-arusi alikuwa Mbinguni wakati ule ule. Wazia hilo!”

³¹⁶ Nilisema, “Bw. Bohanon, jambo ulilo nalo, umechanganisha mambo matatu mbalimbali, ukayaita ‘Bibi-arusi.’ Unawaita wale mia na arobaini na nne elfu waliosimama na Mwana-Kondoo kwenye Mlima Sinai, ‘Bibi-arusi’ hao sio. Unawaita wale . . . Akatoa maji katika kinywa chake kufanya vita na Wazao waliosalia wa mwanamke ambao hawakuwa Bibi-arusi, hao ndio wale waliosalia. Bibi-arusi alikuwa Mbinguni; wale mia na arobaini na nne elfu *pale*; na yule Mkristo kwa jina tu akienda hapa kwenye mateso. Naam.”

³¹⁷ Soma, ndugu, sasa kama umepapata [Ndugu Neville aanza kusoma I Wakorintho 15.29—Mh.].

Au je! Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje? kama . . . [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]

³¹⁸ Roho Mtakatifu aweza kuja hivi sasa tunapozungumza. Roho Mtakatifu ni karama ya Mungu. Ona? Hiyo ni karama ya Mungu, angeweza kuja tugali tunazungumza. Nami nawaambia, wakati . . . kama watu wangelifundishwa vizuri . . . Wengine wenu watu wa zamani hapa, hebu niwaulizeni kitu fulani. Ninyi watu wa zamani, Roho alikuwapo papo hapo kumpokea, nao walipokuja toka majini wakampokea Roho Mtakatifu. Naam.

³¹⁹ Uki . . . Wachungaji, fundisheni kondoo zenu, wapelekeni katika Biblia hapa. Achaneni na hicho kitabu cha kale cha kanisa na rudini papa hapa katika Biblia ambapo Mungu aliongea, na hamtakuwa na shida hizo.

³²⁰ Naam, kwa kuwekwa mikono ndivyo tunavyoweza kumpokea Roho Mtakatifu, mtu mwenye upako akiwekea mikono.

48. Ndugu Bill, je . . . Je, ni taratibu kwa mtu fulani kusimama na kutoa jumbe kwa lugha hali mhubiri anatoa . . . Neno?

Mtu huyu ana maswali matatu hapa, na lingine ni:

49. Pia, ni taratibu kufanya vivyo hivyo wakati wito wa madhabahuni unapotolewa?

Tatu, la tatu:

50. Pia, je, nje ya . . . je, ni taratibu kwa mtu kusimama kanisani na kumpinga mhudumu kwa kitu alichosema au kufanya katika ibada, naye akiwa nyuma ya dawati takatifu? Mambo haya yote yamefanywa Maskanini humu mara kadha.

³²¹ Sasa, hebu niendee haya upesi sana sasa, haya yanahusu kanisa sasa. Mimi . . . Sasa kwenu ninyi mlio wageni malangoni mwetu, yanipasa nilipige kanisa kofi kidogo sasa, ili ninyi—ninyi kaeni mbali kwa dakika moja hivi, mkiweza.

³²² Sikizeni watoto wangu! Karama hizo ni za ajabu. Hakuna ye yote ajuaye jinsi nawathamini, nami nawapaenda kwa

upendo wa kiungu. Lakini karama hizi zinaweza kuwadhuru msipozitumia mahali pake panapofaa.

³²³ Watazame watu siku hizi, watu wazuri huko umisheni, wakiwaombea wagonjwa na kutoza fedha kwa hayo. Hilo ni kosa. Kama mtu ana imani ya uponyaji na kuwaombea wagonjwa, yeye yampasa awe muungwana kutosha kuwaombea watu pasipo pesa. Namshukuru Mungu! Ndugu, nataka kusema hilo, si kwa ajili yangu mimi, lakini kwa utukufu wa Mungu, hakuna hata wakati mmoja ambapo nimechukua pesa toka kwa watu wala cho chote kama hicho; na nikakataa, wazi, dolla milioni, dolla mia tano elfu katika toleo moja. Nanyi mwajua hilo. Ilikuwa papa hapa gazetini. Ona? Naam. Si kwa ajili ya . . . Unapofanya hayo utapoteza imani yako kule kwa Mungu.

³²⁴ Sasa, ninyi watu mnaonena kwa lugha na mna karama za lugha, Mungu awabariki. Mnahitajika katika Maskani haya. Nawatakeni ninyi hapa. Lakini, sasa, kitu ki—kile kiko katika utaratibu, msifanye vile hali mhubiri anahubiri. Mkifanya hivyo, hamko katika utaratibu. Ona? Hampaswi kufanya hilo. Kwa maana Biblia ilisema, “Roho ya manabii humtii nabii.” Na mtu anapohubiri, yeye ameshika kunena, ana wasikizi, Roho Mtakatifu atanena kupitia kwake. Lakini yeye amalizapo, basi wakati ule ni wakati wa ujumbe, waona. Kwa hivyo msiwe bila utaratibu; mkifanya vile, basi mnakatiza nanyi—nanyi mnamhuzunisha Roho Mtakatifu kwa ujumbe unaotolewa.

³²⁵ Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa mkutanoni juu hapa mahali fulani Washington, maelfu mengi ya watu walikuwa wameketi pale. Na msimamizi wangu, ambaye ni mfafanua Biblia halisi, yeye alikuwa amesimama pale akinena kuhusu Uponyaji wa Kiungu, ana upako, Roho Mtakatifu alikuwa akinena. Mwanamke fulani alisimama na akaanza kunena kwa lugha, naye alingoja kwa muda mchache, ndipo akaendelea. Roho Mtakatifu akaanza . . . kuhuzunika, ungeona hilo kati ya watu. Yeye akaanza kunena tena, na mwanamke yule akasimama tena; naye akamwambia, “Dada, keti chini, katika Jina la Bwana.” Kasema, “Uko nje ya utaratibu.” Na wahudumu walimpeleka kule na kumsahihisha.

³²⁶ Sasa, jambo ni kwamba, karama hizo ziko ulimwenguni, ziko kanisani sasa. Karama hizo ziko kanisani lakini watoto wachanga hupokea karama hizo na hawana mafundisho jinsi ya kuzitawala. Kama ungezitumia vibaya, ungefanya dhara zaidi ya vile ungetenda mema. Ona?

³²⁷ Ni kama tu mtu akienda nje, akaombea wagonjwa na mtu fulani akiponywa asema, “Sasa, yakupasa unipe dolla elfu moja kwake.” Sasa, yeye amefanya dhara zaidi ya kutenda mema. Ingekuwa heri kama mtu yule angaliachiliwa afe badala ya kuleta fedheha kama hiyo juu ya Kristo.

³²⁸ Sasa, wakati unapo... Mchangaji au mhubiri, au ye yote yule, anapohubiri, tulia. Paulo alisema afanye hivyo, mwaona. Sasa, na ndipo yeye alisema, “Mnaweza kunena, moja kwa moja.” Hiyo ni kweli kutosha. Naye alisema, “Nami nataka ninyi nyote mnene kwa lugha. Hivyo ni vizuri.”

³²⁹ Lakini huwezi kunena kwa lugha isipokuwa una karama ya lugha. Na bila shaka kuna karama nyingi zake kanisani humu sasa. Kuna karama nyingi zake hapa katika kanisa Methodisti, kunazo nyingi hapa katika kanisa Baptisti, kama ingehubiriwa tu hivyo karama zile zingetenda kazi.

³³⁰ Vipi... Ukipanda mbegu katika ardhi na usiipalilie, itakuwaje? Ona? Itakaa pale katika vumbi kavu na kuoza, haifai kitu. Karama hizi zimekuwa katika kanisa muda huu wote, lakini hivi sasa maji yanaanza kumwagika, ile mvua ya Pentekoste, kuitia maji ikazae matunda. Sasa, itumie mahali panapofaa.

³³¹ Sasa, linasema, vema, naamini swali linalofuata lilikuwa pale, mtu yule aliuliza, kasema:

Unapo... unapotoa wito wa madhabahuni?

³³² La, singedhani wakati huo. Mkichunguza, na kuchukua Wakorintho na kuisoma, kunao wengine wenu hapa, kama—kama mna karama za kunena kwa lugha, basi iweni macho. Katika Biblia walipokuwa na... baada ya ibada kwisha, na baraka za Mungu kushuka juu ya kusanyiko, ndipo wao walianza kunena kwa lugha, kisha wakaanza kumtukuza Mungu. Na kila wakati, ilikuwa ni ujumbe wa moja kwa moja kwa mtu fulani. Si... Yawapasa mchunguze hilo sasa. Ona? Si kitu fulani tu cha kimwili. Itakuwa ni ujumbe kwa mtu fulani, kwa ajili ya mtu fulani kufanya kitu fulani, au kitu fulani cha kujenga kanisa. Kitakuwa kitu fulani cha kulitukuza kanisa.

³³³ Na hapo ndipo Wapentekoste wameleta fedheha kwa jina lao. Na jina lile lile *Pentekoste*, unaweza kulitaja na watu wataondoka na kusema, “Upuzi,” kwa sababu wanaona mengi sana yasiyofaa, ambao ni watu wanyofu lakini hawakufundishwa.

³³⁴ Paulo alisema, “Nitakapokuja huko kwenye kanisa Pentekoste,” kasema, “Nitayatengeneza.” Yapasa iwe katika utaratibu, na kila kitu lazima kifanyike kwa utaratibu, kama Roho alivyoamuru. Kwa hivyo yeye alisema, “Sasa, mkiingia, nanyi nyote mnaanza kunena kwa lugha; na mtu asiye funzwa aingie, yeye atasema, ‘Vema, si ninyi nyote mu wazimu?’ na kuondoka.”

³³⁵ Hayo ndiyo kanisa Pentekoste hufanya. Yeye alisema, “Sasa,” na kusema, “kama mmoja wenu atatoa unabii na kuweka wazi siri za mioyo, mmoja wenu ni nabii,” kwa maneno mengine, yeye alisema, “basi si watu wataanguka chini na kusema ‘Mungu yu kati yenu?’”

336 Vema, ningekanushaje karama ya kunena kwa lugha huku ingenipasa kukana karama ya unabii, itapasa nikane karama hizi zingine zote? Sasa, makanisa mengi sana, makanisa makubwa, Wanazarini, Pilgrim Holiness, na wengineo, wanadhani mtu akinena kwa lugha yeye ni ibilisi. Huko ni kukufuru Roho Mtakatifu, ambako hakuna msamaha. Hayo ndiyo Wayahudi walitenda, wakafanyia mzaha watu waliokuwa na Roho Mtakatifu, nao walihukumikiwa na kupotea kwa ajili ya hayo. Sawa! Je, si Yesu alisema, “Ukinena neno moja dhidi ya Roho Mtakatifu hautasemehewa katika ulimwengu huu wala ulimwengu ujao?” Kwa hivyo jihadhari! Kama hulielewi, tulia kimya.

337 Nanyi watu mlio na Roho Mtakatifu na kuitwa katika huduma, waalimu... Sasa, ungewaza... mimi niko hapa nikijaribu kufundisha, na hapa aruka mtu, kando yangu, na kuanza kufundisha wakati uo huo, mwingine amesimama hapa akiimba wimbo wa siku kuu? Vema, tatanisho vipi!

338 Vema, hivyo ndiyo ilivyo kuhusu kunena kwa lugha. Na ije kwa utaratibu, kama tu vile Roho aitoavyo, unaweza kunena kwa lugha.

339 Sasa unasema, “Vema Ndugu Branham, siwezi kujizuia.”

340 Ee, naam, unaweza! Paulo alisema ungeweza, yeye alisema, “Kama kunaye mmoja kati yenu, anenaye kwa lugha, na asiwepo mwenye kufasiri, na anyamaze.” Haijalishi jinsi inataka kunena, tulia. Hiyo ni karama, ndugu. Ni—ninasema, Mungu aruhusu niwe na mkutano wa ufufuo mojawapo wa siku hizi ili tuweze kuingia katika mambo haya, mpate kuona. Ambapo unaweza kuona ni karama, na karama hiyo inataka kufanya kazi wakati wote. Ona? Lakini yakupasa uwe na hekima ya Roho Mtakatifu hapa kujua wakati upi na jinsi gani utatumia karama hiyo. Na hayo...

341 Unasema, “Vema, Mungu atukuzwe, Biblia ilisema Roho Mtakatifu ajapo huhitaji mwalimu ye yote, Yeye Mwenyewe ni Mwalimu.” Ee, ndugu! Unawezaje kuwa wa chini sana katika kusoma Maandi-... Mbona Roho Mtakatifu aliwaweka waalimu kanisani, basi?

342 Wasema, “Hainipasi kufundishwa na ye yote, Roho Mtakatifu hunifundisha mimi.” Hukufundisha, kupitia kwa mwalimu. Yeye aliweka waalimu kanisani.

343 Yeye alisema, “Je wote ni waalimu, ninyi wote ni mitume, wote wana karama za uponyaji?” Roho Mtakatifu aliweka vitu hivi kanisani, na Yeye huviendesha vyote, na kila moja yavyo hutenda kazi kwa utaratibu.

344 Sasa, ni kama tu mguu wangu; mmoja wayo useme, “Ninaenda huku,” mwingine useme, “Ninarudi nyuma huku.” Sasa, utafanyaje? Mkono unasema, “Nitakwenda juu,” na

mwingine unazunguka hivi. Je, mwili utakuwa na umbo la namna gani? Ona?

³⁴⁵ Lakini, sasa ubongo hapa ukisema, (nini?), “Jongeleeni mbele, ninyi nyote. Mkono, nenda pamoja nao. Kichwa, kaa wima. Mikono, fanyeni vivyo hivyo,” kila kitu kikitembea kwa upatanifu. Sasa, nifikapo kule, sijatumia mikono yangu. Sasa, miguu imetenda wajibu wake, mchungaji amemaliza kuhubiri; sasa, mikono fanyeni wajibu wenu. Ona? Mwafahamu lile ninalokusudia?

³⁴⁶ Vema, vipi kama mikono ilikuwa ikienda hivi, “Ee, kiko wapi? Kiko wapi?” Nawe ukijaribu kukichukua, ona, wewe ungali bado hauko pale. ona? Tulia, mkono. Wakati wako wa kutumika utawadia hivi punde, ngoja hata ufike pale. Mwafahamu ninalokusudia? Hiyo ni karama, hiyo ni karama ya Roho ikifanya kazi.

³⁴⁷ Nampenda Bwana. Nanyi je? Amina. Sikizeni, najua jambo moja ninaloweza kusema juu yenu, hakika mna saburi; saa nne na dakika ishirini. Sasa, marafiki, tazameni hapa hivi sasa. Mimi. . . Hili ni bora kadiri nijuavyo. Yanipasa niharakishe kupitia chungu nzima yayo hivi. Usi. . . usipokubaliana na hilo, usinikasirikie. Uwe ndugu yangu, ona. Nawapenda, nami nasema tu mambo haya kwa sababu hilo limo moyoni mwangu. Hayo ndiyo ninayoamini na hivyo ndivyo mimi hueleza, na hivyo ndivyo mimi ninavyolileta, linatoka kwa Biblia.

³⁴⁸ Sasa, ukisema, “Ndugu Branham, siamini hivyo.” Hilo litakuwa sawa kabisa, ona. Hatutawaza vingine kamwe, tutaendelea tu kama ndugu na marafiki.

³⁴⁹ Na—na ukisema, “Vema, ni—ninaamini nikiwa wa kanisa Methodisti au kanisa Batisti, nitaokoka haidhuru.” Vema, ndugu, hilo ni sawa kabisa. Mimi bado ninakuia “ndugu yangu,” kwa sababu unamwamini Yesu Kristo. Ona? Naam. Kwa hivyo tutakuwa ndugu na marafiki haidhuru.

³⁵⁰ Lakini naeleza tu hili kwa kanisa hili, hizi siku chache hapa, Mafundisho ambayo kanisa hili hushikilia! Ona? Hayo ndiyo kanisa linayosimamia! Na iwapo mna shemasi hapa ambaye haamini katika ubatizo kwa Jina la Yesu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, au kudhihirishwa kwa karama za Roho, shemasi huyo, papa hapa hali nimesimama hapa, hastahili kuwa kanisani hata atakaposahihishwa. Hiyo ni kweli kabisa. Na yapasa halmashauri itekeleze hilo. Hakika! Kanisa hili halisimamiwi na mashemasi; kanisa hili linasimamiwa na Biblia na Roho Mtakatifu, pekee. Naam, bwana. Sasa, mambo hayo, twaamini hayo ni Mafundisho ya kanisa hili.

³⁵¹ Hatuna ufuasi wo wote. Hakuna ye yote aliye mfuasi hapa, lakini ye yote ajaye ni mshiriki, kwa kuwa twaamini kuwa sisi sote tu washiriki wa Mwili mmoja kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

³⁵² Nasi tunawashurutisha, ndugu au dada wapendwa wetu Wakristo, mbatizwe kwa Jina la Yesu Kristo na mpokee Roho Mtakatifu. Kama umekwisha pokea Roho Mtakatifu, baada kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, Mungu akubariki! Unasema, “Ndugu Branham, nifanyeje kuhusu hilo?” Swali hilo lilijibiwa. Naweza kusema tu kama Paulo, yakupasa ubatizwe tena!

³⁵³ Sasa, tazama hapa, Matendo...Hebu nisome haya, Wagalatia 1:9. Iandikeni ninyi mnaoandika. Paulo alisema... Mtu yuyu huyu aliyeyasema haya, aliyefundisha msemu huu. Mwaamini hayo sasa? Sivyo? Paulo alikuwa amewaambia iliwapasa wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo. Na Paulo alisema, “Kama malaika toka Mbinguni...” Wagalatia 1:8, “Kama malaika toka Mbinguni angewafundisha ninyi nyingine yo yote mbali na Hii, na awe kwenu aliyelaaniwa.” Kama yeye ni askofu mkuu, kama yeye ni papa, kama mhudumu fulani, kama yeye ni nabii, kama yeye ni kasisi, kama yeye ni malaika fulani toka Mbinguni, au ye yote yule, yeye alisema, “Wakifundisha lo lote mbali na Hili, na alaaniwe kwenu!” Sivyo? Naye alirudia tena. Yeye alisema, “Kama nilivyotangulia kusema, na sasa nasema tena; wakifundisha lo lote isipokuwa Hii, na walaaniwe!” Sivyo?

³⁵⁴ Kwa hivyo Bwana awabariki. Yasome toka kwa Neno, nanyi jiamulieni

³⁵⁵ Sasa, wangapi wanapenda huo wimbo mzuri wa kale:

Imani yangu imeelekezwa Kwako,
Ewe Mwana—Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi mtakatifu.
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa hatia yangu yote,
Nami tangu leo Niwe Wako Kabisa!

³⁵⁶ Nataka kuwaulizeni jambo fulani, ninyi katika kanisa hili. Kama mtu anayekufa akihubiria watu wanaokufa, nikitambua kuwa huenda haya yakawa mahubiri yangu nitakayowahi kuhubiri; nami najaribu kuhubiri kila mahubiri nihubiriyoy, kama kwamba yalikuwa yangu ya mwisho kama mtu anayekufa kwa mtu anayekufa. Sasa, nawaulizeni ninyi, ndugu zangu, na raia wenzangu wa jumuiia hii na nchi hii, je mnajisikia hakika kuwa mnahitaji kutembea karibu sana Mungu baada ya ibada hizi? Mungu awabariki! Mimi kama ndugu yenu, nikiwazungumzia ninyi, ombi langu la moyoni ni kwenu, kuwa mtapokea huku kutembea karibu sana na Mungu.

³⁵⁷ Na, siku ya Hukumu, ambapo usiku huu mtatu ambapo nimekuwa nikihubiri, itakuwa kama—kama ukanda mkuu ulionaswa ukisikizwa siku hiyo, na sauti yangu itajitokeza, nami itanipasa kusimama pale na kutoa habari zangu mwenyewe, kwa maana maneno yangu yatanibariki au yatanihukumu siku

hiyo. Na hayo yamekuwa maneno yangu kwa miaka ishirini na kitu kama kijana wa umri wa miaka karibu ishirini, nikihubiri Injili, nami nina umri wa miaka arobaini na mitano sasa. Nami sijaigeuza hata kidogo, kwa sababu singeibadili kwa kadiri Biblia idumavyo hivyo.

³⁵⁸ Nimeipeleka kwa maaskofu na kila kitu, nami bado sijaona ambaye angenena kinyume Chake, kulingana na Neno. Wao husema... Vema, sasa, mimi... Kasisi huyu, hapa siku chache zilizopita, yeye alisema, “Kasisi Branham, hatuchukui Biblia, ni kanisa kwetu sisi.” Kwa hivyo huwezi kuongea na mtu huyo. Lakini ukiwekea msingi kwenye Biblia, hilo ni tofauti. Ona?

³⁵⁹ Naomba kuwa Mungu ata... Kila mmoja wa marafiki zangu Wakatoliki ndani humu, na kila mmoja wa marafiki wangu Waprotestanti na hata... Hakuna tena... Yeye yote... Ni—ninapenda tu kila mmoja wenu. Mungu ajua kama hilo ni kweli au sivyo. Tazama katika mstari wa wanaohitaji maombi, wakati vipofu... vipofu na viwete, haisemi, “Katoliki.”

³⁶⁰ Hapa yuaketi mtu papa hapa juk-... papa hapa, Mkatoliki, akifa kwa ugonjwa wa kansa, imemla; yeye alikuja nyumbani kwangu na Roho Mtakatifu akamshukia, akamponya. Yeye hakuniambia kamwe kama alikuwa Mkatoliki au la; sikumwambia neno kamwe. Yeye alikuja na akabatizwa kwa Jina la Yesu Kristo na kumpokea Roho Mtakatifu. Mtu huyo anaketi pale, mfanyi biashara Louisville... Louisville...?...

³⁶¹ Yeye haulizi kama wewe u Mkatoliki au la, ni kama moyo wako una njaa ya Mungu. “Heri wenye njaa na kiu cha haki, maana watashibishwa.” Sivyo? Amina. Bwana awabariki.

³⁶² Wangapi wanaoujua huu wimbo mzuri wa zamani, *kibarikiwe Kifungo Kitufunganishacho*? Watu wangapi hapa wana umri unaozidi miaka arobaini, inueni mikono yenu pamoja nami mkaseme, “Nakumbuka huu wimbo wa zamani, tangu miaka arobaini, *Kibarikiwe Kifungo Kitufungiacho*.”

Kibarikiwe kifungo kifunganishacho
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye nia moja
Unafanana na wa kule juu.

³⁶³ Je, hamzipendi hizo nyimbo za kale? Sikiza, nataka kusema haya, kama tungekuwa na wingi wa hizo nyimbo za kale badala ya hizi nyingi mno zisizofaa tulizo nazo, naamini kanisa lingekuwa bora zaidi. Napenda hizo nyimbo nzuri, za zamani, zilizoandikwa na Roho Mtakatifu, hao watu wa zamani.

³⁶⁴ Nilikuwa nikikumbuka mzee mmoja mweusi, alikuwa akiketi nyuma ya nyumba, kule chini katika milima ya Kentucky. Yeye alipochoka, angeketi juu ya hilo gogo kuukuu sana na kupigapiga hilo gogo kwa mikono yake. Namkumbuka vema tu... Alikuwa na mzingo mdogo wa mvi kichwani mwake. Aliuimba huo wimbo wa kale, wimbo wa zamani.

Nitainuka niende kwa Yesu
Atanikumbatia katika mikono Yake;
Mikono mwa mpendwa Mwokozi wangu,
Ee, kuna haiba kumi elfu.

³⁶⁵ Hauna sauti nzuri sana. Wangapi wamepata kuusikia huo
wimbo wa zamani? Naam. Sikizeni...[Nafasi tupu kwenye
ukanda—Mh.].



Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org